SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Atuhumiwa** kuua mke, amzika juu ya shimo apanda mpunga

UKURASA 3



**POCHETTINO ALIA NA KIWANGO KIBOVU**

UKURASA 22

Nipashe
Jumatatu Machi 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580877
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Mbowe afunguka

• **Atoa** shukrani kanisani, aeleza miezi 8 ya maisha yake gerezani, kuzungumza na Watanzania... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akizungumza wakati akitoa shukrani katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Azania Front jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### UNFPA YACHANGIA SENSA DOLA MIL. 2/-

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), limechangia Dola milioni 2.187 za Kimarekani kwa ajili ya kusaidia kufanikisha...

UKURASA WA 4

### WAFUNGWA CHADEMA WALISHUKURU NIPASHE

WANACHAMA wanne wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kata ya Majengo, Halmashauri ya Mtama, Wilaya...

UKURASA WA 5


### SUDAN YAHITAJI TANI 10,000 MTAMA WA TANZANIA

TANZANIA imeshindwa kupeleka tani 10,000 za mtama zinazohitajika nchini Sudan Kusini kutokana na wakulima wengi kuuza kwa wanunuzi...

## Wanaume wanaopigwa na wake zao watoa kilio

UKURASA 3


Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store



## Neema yaja kwa wagonjwa wa figo

UKURASA 9

MICHEZO **SIMBA HESABU KWA BERKANE** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, akisalimiana na mmoja wa kinamama wa Kata ya Vigwaza kwenye ziara yake katika Jimbo la Chalinze, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Freeman Mbowe afunguka

**Na Waandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ameelezea maisha yake ya miezi minane alipokuwa mahabusu katika Gereza la Segerea mkoani Dar es Salaam.

Mbowe na wenzake watatu waliachiwa huru mwishoni mwa wiki baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha taarifa mahakamani ya kutokuwa na nia ya kuendelea na shauri hilo.

Mbowe alifutiwa mashtaka baada ya kukaa gerezani siku 227 akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi pamoja na kupanga matukio ya ugaidi.

Akizungumza jana katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Azania jijini Dar es Salaam alipokwenda kutoa shukrani, Mbowe pamoja na mambo mengine, alikuwa akipokea wageni wengi kwa siku, hali iliyowashangaza maofisa wa Magereza.

Alisema kuna siku alipokea wageni 214, hali iliyolazimika maofisa wa Magereza kumtengea sehemu maalum ya kuzungumza nao.

Katika ibada hiyo, Mbowe alizungumzia namna watu waliokuwa wakimtembelea akiwa gerezani, akidai kuwa idadi ya waliomtembelea ilivunja rekodi.

"Ilikuwa nikianza saa tatu asubuhi mpaka saa tisa tunapofungiwa nakuwa na mgeni mmoja baada ya mwingine ikalazimika kuweka kumbukumbu ya mahudhurio kwa wageni wote wanaokuja kunipa pole watu wamelia na mimi nimeona machozi mengi furaha na vicheko vingi," alisema Mbowe.

Alisema miezi minane aliyokaa gerezani haikupotea bure bali alipata muda mwingi wa kusoma na kuandika, huku akieleza alikuwa na amani na furaha kwa wakati wote kwa sababu ni miujiza mingi imefanyika katika kipindi alichokuwa gerezani.

"Watu walikuwa wanatoka Kigoma kwa mabasi tena ya kukodi kuja kuniona wengine Kagera, Kyela," alisema Mbowe.

**AKATAA KESI KUFUTWA**

Mbowe alisema japokuwa Watanzania wengi wakiwamo viongozi wa dini na siasa walikuwa wanaomba mara kwa mara kuwa kesi hiyo ifutwe, lakini yeye alikuwa anaomba isifutwe hadi ukweli ujulikane.

Mbowe alisema: "Watu wengi walikuwa wanaomba mara kwa mara mtoeni Mbowe futeni mashtaka, lakini mimi mwenyewe nilikuwa naomba yasifutwe hadi ukweli udhihirike."

Aliongeza: "Nilitamani nisikie hao walionituhumu kwa ugaidi watatoa ushahidi upi ili dunia ielewe kwa sababu kulikuwa na mahakama ya mahakamani na mahakama ya umma."

Mbowe alisema alishtakiwa kwa kosa kubwa ambalo kifungo chake si chini ya miaka 30 na hakuna faini.

"Kwa hiyo ni kosa ambalo unaweza kufungwa maisha, lakini nilimwomba sana Mungu anisaidie dunia ijue ukweli kuhusu jambo hili natambua wako wengi ambao walishtuka na wakahisi Mbowe amefanya kitu fulani," alisema Mbowe.

"Nimejifunza mengi, wengi walitegemea atatoka na hasira na chuki, Mungu alinipa ufunuo nifurahi na kila mmoja na kutengeneza amani na kila mmoja hata nilipopata ujumbe wa Rais Samia Suluhu Hassan kuonana naye nilikubali kwenda," alieleza.

**KUZUNGUMZA NA TAIFA**

Kadhalika, Mbowe alisema muda mwafaka ukifika atazungumza na Watanzania kiundani kuhusu mkasa wote ulivyotokea.

Alisema anachokifanya kwa sasa kwenye siasa ni wito, kwamba hafuati fedha wala cheo.

"Ninachoweza kusema ni asante kwa upendo wenu, tambueni miezi ninane nimejifunza kwa mambo mengi. Wengi walifikiri baada ya kutoka gerezani nitakuja na hasira, chuki."

Mbowe alisema saa chache baada ya kutoka gerezani, alipata ujumbe wa kuzungumza na Rais Samia Suluhu Hassan, na alikubali kwenda na kwamba wengi walihofu atazungumza nini.

Alisema: "Kuna mengi nimejifunza nilipokuwa gerezani. Sijutii hata siku moja. Nitaongea na Taifa. Nilikuwa na mambo mazito ya kumweleza Rais Samia Suluhu Hassan nashukuru nimemweleza na yeye amekubali kuyafanyia kazi."

"Nchi yetu imejawa na hofu nyingi unaogopa kwamba nikionekana na fulani nitaonekana msaliti. Kifupi sana nilipoonana na mama (Rais)... sisi kama Taifa tafsiri 'narrative' kuzungumza amani kuna watu wengi hawana amani. Na nilimwambia mheshimiwa Rais".

"Wengi hawana amani. Haki katika siasa, utumishi, dola, nashukuru Rais Samia alikubali hili tulilizungumza. Haki ikiwapo amani huja 'automatic' kuna watu hata kusalimiana wanaogopa. Siasa isitugawe ni kitu cha kutupeleka katika ni mafanikio ya kulipeleka Taifa.

"Nikamwomba mama (Rais Samia) kwamba hii amani kuna wengi hawana. Tukihubiri 'justice' (haki) wengi watakuwa na amani. Tuhubiri neno haki, ili nchi iwe salama na mahala pa kuishi."

■**Imeandaliwa na Christina Mwakangale na Gwamaka Alipipi**

# UNFPA yachangia sensa Dola mil. 2.19/-

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), limechangia Dola milioni 2.187 za Kimarekani kwa ajili ya kusaidia kufanikisha zoezi la sensa ya watu na makazi.

Hayo yalisemwa na Naibu Mwakilishi Mkazi wa shirika hilo nchini, Dk. Wilfred Ochan, katika warsha ya waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi.

Warsha hiyo ilikuwa ni sehemu ya maadhimisho kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani itakayofikia kilele chake kesho.

Dk. Ochan alisema, gharama ya bajeti ya sensa hiyo ni Dola za Kimarekani milioni 272.275 na kwamba kati ya hizo, UNFPA imechangia Dola milioni 2.187.

"Tutaendelea kufanya kazi kwa karibu kusaidia serikali ya Tanzania kufanikisha sensa kwa kila Mtanzania kuhesabiwa," alisema Dk. Ochan.

Alisema takwimu za sensa ni chanzo muhimu cha kupata taarifa za mambo ya jinsia hata zile ambazo zimejificha, ambapo ametaka jamii ijengewe uelewa kuhusu umuhimu wa sensa hiyo. "Hivyo tuungane kuijengea jamii uelewa kuhusu sensa ijayo ili kuhakikisha kila mmoja anaelewa umuhimu wake ili awe tayari kuhesabiwa kwa manufaa yake na taifa kwa ujumla," alisema.

Alisema, hatua hiyo ni muhimu pia kusaidia kuijenga Tanzania ambayo wananchi wenyewe wanaitaka, hivyo aliwataka wadau wote kuungana na serikali kuhakikisha sensa inakuwa na mafanikio.

Ofisa miradi, idadi ya watu na maendeleo wa shirika hilo, Ramadhan Hangwa, alisema, kila sensa inaendelea kubadilika kadri miaka inavyokwenda.

"Kwa mfano, miaka ya nyuma hakukuwa na dodoso la watu wenye ulemavu, lakini sasa limewekwa na mengine ya msingi, hivyo kuhesabiwa ni jambo la muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi na watu wake," alisema Hangwa.

Aidha, alisema sensa si jambo la kulazimisha bali kukaa na kuemilisha jamii, kwa maelezo kwamba, iwapo wananchi wakilazimishwa kuhesabiwa, wanaweza kutoa takwimu zisizo sahihi.

Alifafanua sehemu kubwa kwenye sensa ni utoaji wa elimu kwenye jamii, na kwamba kwa kiasi kikubwa, jamii imeanza kuwa na uelewa.

"Ninasema hivyo, kwa sababu miaka ya nyuma kulikuwa na watu wasiotaka kuhesabiwa na sababu kubwa ni uelewa mdogo kuhusu sensa, lakini sasa ninaamini kuwa sensa ya mwaka huu watu wengi wanaweza kujitokeza kuhesabiwa, kwani elimu inaendelea kutolewa," alisema.

Mratibu huyo aliwataka waandishi wa habari kusaidia kutoa elimu kwa umma kupitia taarifa wanazozitoa ili kufanikisha sensa hiyo inayotarajiwa kufanyika Agosti 22, mwaka huu.

## HABARI KITAIFA

# Atuhumiwa kuua mke, amzika juu ya shimo apanda mpunga

**Na Hamisi Nasri,**
TANDAHIMBA

MKAZI wa Tandahimba mkoani Mtwara, Shaibu Kuselela, anatafutwa na polisi kwa tuhuma ya kumuua mkewe na kitu kinachodhaniwa kuwa na ncha kali na baadaye kumzika kwenye shamba na kupanda mpunga ili kupoteza ushahidi.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapo, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, ACP Nicodemus Katembo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa limetokea Februari 28, mwaka huu, katika kijiji cha Lipalwe mkoani humo.

Alisema kuwa mwanamume huyo alifanya unyama wa mauaji hayo ya mkewe Amina Mtausi (40) kwa kutumia kitu kinachodaiwa kuwa na ncha kali.

Alieleza baada ya kutekeleza mauaji hayo aliuchukua mwili wa marehemu na kwenda kuufukia katika shimo shambani kwao kisha kuchukua mpunga na kuupanda juu ya shimo hilo.

Pia, baada ya kutekeleza azma yake alitoweka kusiko kujulikana kutokana na kuhofia kukamatwa na vyombo vya sheria na chanzo cha mauaji hayo hakijajulikana. ACP Katembo alisema tukio hilo limegundulika juzi baada ya mdogo wa mtuhumiwa huyo, Omari Saidi, alipokuwa akienda kisimani kuchota maji katika shamba hilo na kubaini harufu isiyo ya kawaida.

Alisema alipofuatilia kujua ni kitu gani ambacho kilikuwa kikitoa harufu na aliona baadhi ya viungo vya marehemu huku sehemu ya mwili ukiwa umefukiwa ndani ya shimo.

ACP Katembo alisema, Saidi alitoa taarifa kwa vyombo husika kwa ajili ya kufuatilia tukio hilo kwa kina zaidi.

Jeshi la Polisi mkoani Mtwara lilifika katika eneo hilo la tukio wakiambatana na madaktari kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu wa mwili huo na hatimaye baada ya vipimo ulibainika kuwa na majeraha ya kuchomwa na kitu chenye ncha kali sehemu za kisogoni na kutokwa na damu iliyosababisha kupoteza maisha.

Alisema Jeshi la Polisi bado linaendelea kumsaka mtuhumiwa huyo ili afikishwe katika mahakama kwa ajili ya kujibu tuhuma zinazomkabili za mauaji.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, akieleza jambo katika ukaguzi wa miundombinu ya barabara wilayani Ileje mkoani Mbeya juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaume wanaopigwa na wake watoa kilio

**Na Renatus Masuguliko**, GEITA

BAADHI ya wanaume wanaodai kutendewa vitendo vya ukatili na wake zao ikiwamo kupigwa na kunyimwa unyumba wamejitokeza kwa wingi katika dawati la jinsia na watoto wilayani na mkoani Geita.

Wanaume hao wamefika katika dawati hilo wakieleza kilio chao na kuomba kupatiwa ufumbuzi ikiwamo ushauri wa kisaikolojia.

Mratibu wa dawati la jinsia na watoto Wilaya ya Geita kutoka Jeshi la Polisi, Sajenti Hidaya Mrisho, aliyasema hayo wakati akitoa mada katika kongamano la wanawake Mkoa wa Geita.

Akitoa mada hiyo juzi katika kongamano hilo Sajenti Hidaya Mriso alisema kuna wakati amekuwa akilengwa na machozi anapopokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya kinababa wanaofika kutoa malalamiko yao kwenye dawati hilo.

Alisema busara hutumika kuyapatia ufumbuzi na kila kinachojadiliwa hubaki kuwa siri ya wahusika tu.

"Kumekuwapo na kukosekana kwa ufahamu kwani wengi wanadhani dawati la jinsia na watoto ni kwa ajili ya wanawake na watoto peke yao, wakati dawati hilo ni kwa ajili ya jinsia zote hii inasikitisha sana. Wapo baadhi ya wanaume wanaona aibu kujitokeza, naomba wajitokeze kama wengine walivyojitokeza na kudai wamekuwa wakipigwa na wake zao, kunyimwa unyumba," alisema.

Alisema kuna baadhi ya kinababa wanaoamriwa na wake zao kufua nguo zao za ndani zikiwamo nguo za kujisitiri. Sajenti Hidaya aliongeza kuwa iwapo usawa utazingatiwa kwa kila mmoja kutimiza wajibu na majukumu yake katika familia itasaidia katika furaha, maadili na kujenga famiia zenye maadili ya kijamii.

Wakili Walter Ghalos, akizungumza katika kongamano hilo alisema tafsiri ya ndoa kisheria ni mktaba wa muungano wa hiari kati ya mume na mke kuishi pamoja maisha yao yote.

Alisema lakini inapotokea uhiari ukakoma kwa mmoja kati yao basi hakuna mkataba tena hatua ambayo ndipo misaada ya kisheria huanza ili kutafuta talaka na hapo ndipo mfarakano huanza busara isipotangulia.

Mtoa mada mwingine, Adelina Kabakama, alisema kuwa haki ya kijinsia ni kwa pande zote lakini kutokana na mila na mfumo dume umechangia wanawake kuwa ndiyo wahanga wa matukio ya ukatili wa kijinsia na watoto.


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

### TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala-Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala-Lugala na Nala-Segu kuwa muda wao wa kulipia viwanja hivyo umeisha. Aidha, katika kuwawezesha kukamilisha malipo hayo, amewaongezea muda hadi tarehe 27.03.2022.

Baada ya kukamilika kwa muda huo, viwanja ambavyo vitakuwa bado vinadaiwa vitarudishwa sokoni ili wateja wengine wavinunue bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji, DODOMA**

216731401



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**INAYOKETI DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA.560/17 YA 2017**

1. FREDY KWEKA
2. JULIUS MUKAMA @ JULIUS BONIFACE MUKAMA
3. EMMA CHARLES MAPUNDA
4. JAQUELINE HERBERT NYAMUGALI

........WARUFANI

DHIDI YA

1. ABDALLAH NJEMA (Deceased) THE ADMINISTRATOR OF ESTATE OF ABDALLAH NJEMA (IF ANY)
2. ALI MOHAMED KAJUNIA

............... WAJIBU MAOMBI

KWA:

1. ABDALLAH NJEMA (Deceased) THE ADMINISTRATOR OF ESTATE OF ABDALLAH NJEMA (IF ANY)
2. ALI MOHAMED KAJUNIA

**POPOTE MLIPO**

Mnajulishwa kwamba shauri la Rufaa ya Madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es Salaam tarehe 30/03/2022 saa tatu kamili asubuhi (3:00).

Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hamtahudhuria nyinyi wenyewe au mwakilishi wenu anayetambulika kisheria basi rufaa itasikilizwa bila ya uwepo wenu.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo hii tarehe 01/03/2022.

L. KALEGEYA
K.n.y: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

# Mabweni ya watoto wenye ulemavu yazingirwa maji, walala madarasani

**Na Ida Mushi**, MOROGORO

WATOTO wenye ulemavu wa akili na walio na mahitaji maalum wapatao 40 wanaolelewa katika kituo cha malezi cha Mehayo (Mental health youth), wanalazimika kulala kwenye madarasa baada ya mabweni waliyokuwa wakitumia kuzingirwa na maji yanayosababishwa na kunyanyuliwa kwa barabara iliyokatiza mbele ya kituo hicho.

Timu ya waandishi wa habari iliyofika kituoni hapo ilishuhudia maji na udongo ukiwa umejaa katika mabweni hayo, hali inayotishia usalama wa afya yao kutokana na kuwa hatarini kushambuliwa na magonjwa.

Kaimu Mkurugenzi wa kituo cha Mehayo, Melkzedeck Saera, amekiri hali mbaya kwa watoto hasa kushambuliwa na magonjwa ya mara kwa mara ya malaria tangu mwishoni mwa mwaka jana, baada ya kutengenezwa kwa barabara hiyo na kuziba mitaro iliyokuwa imeelekezwa kutoa maji nje ya kituo, badala yake maji yote wakati wa mvua huingia ndani na kujaa kwenye mabweni na vibanda vya biashara walivyokuwa wakivitumia kama kitega uchumi.

"Kituo kina changamoto nyingi sana, lakini kikubwa sana sasa kinachotuumiza ni maji, tumeshawasilisha maombi yetu ngazi ya mtaa, kata na kila mahali, kuona namna watakavyoweza kutusaidia ili kuondokana na hii kero, wanafunzi tumewahamishia madarasani, wengine wakubwa kama 30 tumewagawa kwenda eneo letu jingine la Mkundi ambalo licha ya kuwa bado hapajakamilika vizuri, imewalazimu waanze kupatumia, na wengine hawa 40 wadogo wenye umri wa miaka sita na kuendelea ndiyo tumebaki nao hapa wakilala madarasani na kwenye nyumba za watumishi," alisema Saera.

Kaimu Mkurugenzi huyo ameiomba serikali na wadau wengine kusaidia namna bora ya kuondoa maji hayo na kuruhusu kutoka mvua ikinyesha ili watoto hao wenye mahitaji maalum waendelee kuwa salama katika eneo hilo.

Alisema watoto wenye umri mdogo wameendelea kubaki kituoni hapo kutokana na kusoma katika shule jirani ya Mazimbu, ambayo ina madarasa maalum kwa ajili ya wenye mahitaji maalum, wamekuwa wakienda kusoma asubuhi hadi saa tano na kurudi kituoni kuendelea na shughuli zingine za ujifunzaji kama kazi za mikono, shamba na bustani, mazoezi na shughuli zingine.

Waandishi wa habari walifika kituoni hapo kwa kushirikiana na kundi la wanawake wafanyakazi kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE) kituoni hapo, kwa ajili ya kuwajulia hali watoto na kuwapatia mahitaji mbalimbali ya kibinadamu ikiwa ni sehemu ya kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani inayoadhimishwa Machi 8, kila mwaka.

Mwenyekiti wa TUGHE wanawake Mkoa wa Morogoro, Noves Nkwera, alisema jukumu la malezi ya watoto wenye mahitaji maalum linapaswa kufanywa na kila mwananchi kwa kuangalia eneo au mtaa anaoishi, kwasababu watoto hao wanahitaji kuishi kama wengine licha ya kukosa uwezo huo au kuwa na mahitaji maalum.

Aliwahimiza wananchi kupeleka mahitaji kwa watoto hao wenye mahitaji maalum ambao wengine walitupwa na wazazi, walitengwa, wazazi kukosa uwezo wa kuwahudumia.

"Wapo pia baadhi ya wazazi wanaoficha watoto wa aina hiyo kwa hofu ya namna ambavyo jamii itamchukulia, nawasihi wawafichue wawape huduma, kwani nao wana haki ya kufurahi, haki ya kusoma, haki ya kutambuliwa na kupata mahitaji yote muhimu kama ilivyo kwa watoto wengine," alisema.

Baadhi ya watoto katika kituo hicho, Happy John na Alex Gervas, walishukuru kwa msaada huo ambao utasaidia ustawi wa watoto hao kituoni hapo.

Kituo hicho kilianzishwa na Mwalimu Linda Ngido, awali kilipokea vijana wenye ulemavu wa akili kwa lengo la kuwafunza mbinu, stadi na ujuzi mbalimbali wa kukabiliana na hali waliyo nayo, lakini kutokana na mahitaji na maombi ya jamii, waliamua kuendelea kupokea na watoto wadogo na hali hiyo ilimgusa baada ya kufundisha shule mbalimbali za msingi ikiwamo Chamwino, Mwere, Mkundi katika shule yenye mkondo maalum wa wenye ulemavu.



Mafundi wakijenga msingi wa wodi ya mama na mtoto kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kisiwa cha Rukuba, Musoma Vijijini mkoani Mara juzi, ikiwa ni mkakati wa kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TEMESA yapewa mwezi kubadilika kiutendaji

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (sekta ya ujenzi), Balozi Aisha Amour, atoa mwezi mmoja kwa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) kubadilisha utendaji kazi wao na kuleta matokeo chanya katika kutekeleza majukumu yao.

Alitoa agizo hilo jana alifanya ziara katika ofisi za wakala huo, pamoja na mambo mengine aliongea na watumishi na kukagua eneo la kivukoni na karakana ya Songoro iliyoko Kigamboni jijini Dar es Salaam inayokifanyia ukarabati kivuko cha MV. KAZI.

Balozi Aisha aliwataka TEMESA kusimamia nidhamu katika utendaji katika kitengo cha matengenezo ya magari, kwani ndiyo iliyobeba taswira ya wakala, hivyo wahakikishe magari yanayotengenezwa yanakidhi thamani ya fedha ili kuepuka malalamiko ya wateja.

"Hakikisheni mnajipanga upya kwenye ukaguzi wa vivuko ili kuepusha kupeleka vivuko vikiwa kwenye uharibifu mkubwa na kwa upande wa magari hakikisheni mnatumia vipuri vyenye ubora unaotakiwa," alisema Balozi Aisha.

Alisema mwezi mmoja aliowapa wautumie katika kujipanga ili kuhakikisha gharama za kutengeneza magari zinapungua na kuendana na matengenezo wanayofanya na pia kuangalia upya rasilimali watu kama inakidhi mahitaji yao.

"Punguzeni kufanya kazi kwa mazoea na watumishi wanaoharibu taswira ya TEMESA wachukuliwe hatua," alisema Balozi Aisha.

Aidha, aliwapongeza kwa hatua ya haraka waliyochukua kupeleka kivuko cha MV.KAZI kwenye matengenezo ili kuepusha madhara ambayo yanaweza kutokea endapo wangechelewa kukifanyia ukarabati.

Alisema serikali inatarajia kutenga fedha za manunuzi ya kivuko kipya kitakachotoa huduma katika eneo la Magogoni na Kigamboni mkoani Dar es Salaam, ikiwa ni ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwa ni mkakati wa serikali wa kuboresha huduma eneo la Kigamboni.

" Kivuko hicho kitakuwa na uwezo wa kubeba tani 500 sawa na abiria 2,000 na magari 60 na tayari fedha zimeshatengwa kwenye bajeti ya serikali ya mwaka wa fedha 2022/23", alisema Balozi Aisha.

Awali akitoa taarifa kwa katibu mkuu, Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Lazaro Kilahala, alisema serikali imefanya maboresho ya ukataji tiketi kwa kusimika mfumo mpya wa kielektroniki (N-CARD) wa kusimamia mapato katika eneo hilo.

# Wafungwa CHADEMA waishukuru Nipashe

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANACHAMA wanne wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kata ya Majengo, Halmashauri ya Mtama, Wilaya na Mkoa wa Lindi, waliohukumiwa adhabu ya kifungo gerezani, wameshukuru jitihada zilizoonyeshwa na Chama cha ACT-Wazalendo na gazeti la Nipashe.

Shukrani hizo zilitolewa na wafungwa hao mbele ya uongozi wa ACT- Wazalendo ulipowatembelea gerezani kuwajulia hali na mazungumzo ya awali yaliyokuwa na lengo la kujiandaa kuwakatia rufani kupinga adhabu hiyo.

Wakizungumza mbele ya msafara wa viongozi hao, uliokuwa ukiongozwa na Katibu wake, Rashidi Ndauka, wafungwa hao Rajabu Hassani, Moshi Hamisi, Dadi Shayo na Hamisi Maleje, walisema wanawapongeza kwa moyo waliouonyesha.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Rajabu Hassani alisema kufuatia tamko la ACT kutaka kukata rufani kuwanusuru na adhabu ya kifungo gerezani na vyombo vya habari husussan Nipashe kuwapazia sauti, kumewazindua viongozi wa CHADEMA kuanza mchakato wa rufani.

"Sisi taarifa hizi tumesikia kupitia kipindi cha usomaji magazeti asubuhi, ndipo tukaona gazeti la Nipashe limeandika, tumejisikia faraja sana," alisema Hassani.

Walisema kufuatia taarifa hiyo ya ACT-Wazalendo na gazeti la Nipashe kuwapazia sauti, kumesaidia kuwafanya viongozi wao wa CHADEMA kuanza mchakato wa kushughulikia masuala ya rufani yao ikiwamo kuwatembelea gerezani kuwajulia hali.

Naye Katibu wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Lindi, Rashidi Ndauka, akizungumza kwa niaba ya msafara alioongozana nao, aliwataka wanachama hao kutokata tamaa, kwani ni sehemu za changamoto zinazowapata wanasiasa wengi duniani katika kupigania haki kwa jamii.

"Ipo mifano mingi hapa duniani kwa wanasiasa kufungwa magerezani wanaojitokeza mbele kupigania haki zaa jamii," alisema Ndauka. Ndauka alimtaja Rais mzalendo wa kwanza wa Afrika Kusini, Hayati Nelson Mandela kuwa miongoni mwa viongozi maarufu duniani waliokumbwa na kadhia ya aina hiyo.

HABARI KITAIFA

# Sudan yahitaji tani 10,000 za mtama kutoka Tanzania

**Na Faustine Feliciane,**
DODOMA

TANZANIA imeshindwa kupeleka tani 10,000 za mtama zinazohitajika nchini Sudan Kusini kutokana na wakulima wengi kuuza kwa wanunuzi wa ndani.

Kwa mujibu wa Mwakilishi wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) ofisi ndogo za Dodoma, Neema Sitta, wilaya sita zinazozalisha zao hilo katika mradi wa Shirika hilo, zilizalishwa tani 28,000 ambazo ziliuzwa nchini huku mahitaji yakiwa makubwa na kushindwa kupeleka nchini Sudan Kusini tani 10,000 zilizohitajika.

Neema alisema wamepokea oda ya tani hizo kupeleka nchini humo, lakini wameshindwa kufikia tani hizo kwa kuwa wakulima wengi waliuza mtama wao kwa wanunuzi wa ndani.

"Soko limekuwa kubwa kwa sasa mahitaji yanazidi uwezo wa kuzalisha, Sudan Kusini wanataka tani 10,000, lakini hawajapata kwa sababu wanunuzi wa ndani walishanunua mtama wote kutoka kwa wakulima kwenye wilaya zote sita zilizoko ndani ya mradi wa kilimo himilivu cha mtama," alisema Neema.

Alisema kuwa Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) ndiyo wanunuzi wakubwa wa ndani wa mtama na wamesaidia kuendesha kilimo cha mkataba kwa wakulima na kuongeza thamani ya zao hilo.

"Kwa sasa TBL na Msafirishaji Ali Juma, ndiyo wanunuzi wakubwa wa mtama, lakini pia ukiondoa Sudan Kusini wanaohitaji mtama pia Kampuni ya Bia ya Burundi wanahitaji sana mtama kutoka Tanzania," alisema Neema.

Akifafanua alisema kuwa TBL kwa msimu uliopita walinunua tani zaidi ya 8,000 za mtama huku Ali Juma akisafirisha tani 20,000.

"Mahitaji sokoni bado makubwa sana, kwa mfano kampuni ya Bia ya Burundi peke yao wanahitaji tani kuanzia 5,000 sasa mahitaji ya wanunuzi wote ukiunganisha unaona bado uzalishaji haufikii mahitaji ya sokoni," alisema Neema.

Alisema kwa sasa WFP kwa kushirikiana na Shirika la Farm Afrika wanaendelea kuwahimiza na kutoa elimu kwa wakulima kufuata njia za kuongeza uzalishaji wa zao hilo ili kufikia mahitaji sokoni.

Msimamizi wa mradi wa kilimo himilivu cha mtama kwa Wilaya ya Kongwa kutoka Shirika la Farm Afrika, Meshack Panga, alisema wanaendelea na juhudi za kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

"Hii ni fursa nzuri sana kwa wakulima wa hapa Kongwa, lakini kwa wilaya nyingine zinazotekeleza huu mradi, mahitaji ni makubwa sana sokoni kwa hiyo ni juhudi na maarifa ya mkulima katika kuongeza uzalishaji zitamhakikishia kumpa kipato zaidi," alisema Panga.

Mkulima wa zao hilo wilayani humo, Julius Magara, alisema kuwapo kwa uhakika wa soko wa zao hilo kunawapa hamasa ya kulima kwa mbinu bora zaidi kuongeza kipato.

"Kipindi cha nyuma wakulima walikuwa hawazalishi sana mtama kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa soko, kwa sasa hivi tangu ujio wa WFP na Farm Afrika soko ni kubwa sana na bado hatukizi mahitaji yake, kila mmoja sasa hivi tunaolima mtama tunatafuta njia ya kuongeza uzalishaji kwa sababu ya uhakika wa soko," alisema Magara mkulima wa kijiji cha Sagara B.

Ofisa Kilimo wa wilaya hiyo, Mwambungu Keshasi, alisema elimu wanayopata wakulima hao imeongeza tija kwenye uzalishaji.

"Kama Ofisa Kilimo naona manufaa ya mradi huu unaoendeshwa na WFP na kusimamiwa na Farm Afrika, umeleta mageuzi makubwa sana kwenye kilimo cha mtama," alisema.

# Wasichana 3,118 waliokatisha masomo ya sekondari kurejea

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WASICHANA 3,118 wenye umri kati ya miaka 13 na 21 waliokatisha masomo ya sekondari kwa sababu mbalimbali, ikiwamo ujauzito wamejisajili kuendelea na masomo kupitia mradi wa kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari (SEQUIP) unaendeshwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW).

Wasichana hao wananufaika na mradi huo wa miaka mitano kuanzia mwaka 2021 mpaka 2026 unaoendeshwa na serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Mkurugenzi wa Tasisi hiyo, Dk. Michael Ng'umbi, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa Baraza la 12 la Wafanyakazi wa TEWW, mjini Morogoro.

Alisema kuwa kusajiliwa kwa wasichana hao ambao walikatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ugonjwa, hali duni ya maisha na kupata ujauzito umevuka lengo tarajiwa.

Dk. Ng'umbi alisema kila mwaka wa masomo lengo ni kuandikisha wasichana 3,000, lakini idadi hiyo imeongezeka kufikia wasichana 3,118 sawa na asilimia 103.9 na hiyo imetokana na mwitikio wa wasichana hao na wazazi kuona umuhimu wa elimu.

Alisema umelenga kuwafikia wasichana wapatao 12,000 nchini kote kwa kipindi cha miaka mitano ili kuendelea na masomo waliokatisha kutokana na sababu mbalimbali.

Kwa upande wa kuendesha na kusimamia elimu mbadala nje ya mfumo wa shule, Dk. Ng'umbi, alisema taasisi hiyo imeweza kuandaa mitaala na kuendesha programu mbalimbali kwa kutumia mfumo huria na masafa ili kuwafia walengwa walio wengi zaidi nchini.

Alisema programu hizo ni pamoja na elimu ya kisomo na ufundi wa awali (IPOSA), elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi na ufundi wa awali (IPPE), na kwamba kupitia miradi hiyo vijana wapatao 5,000 nchini wameanza kuhitimu mafunzo ya ujuzi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Eliamani Sedoyeka, aliwahakikishia kuwa serikali itatoa fedha kwa wakati ili kazi zote zitakazokubalika katika mpango wa miradi zitekelezwe kwa wakati na ufanisi.

Katika hotuba ilisomwa na Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, Prof. Sedoyeka, alishauri TEWW kuendelea kutafuta vyanzo mbadala vya mapato ambayo yatasaidia katika uendeshaji wa miradi na kutatua changamoto walizonazo.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tanzania inataka nafasi nne CAF, Simba zipiganieni tena

**WAWAKILISHI** pekee wa Tanzania katika michuano ya kimataifa, Simba, leo watashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuikaribisha Dodoma Jiji FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara kabla ya Jumapili kushuka tena dimbani hapo kuialika RS Berkane ya Morocco katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba ambayo imetoka kushinda mabao 3-0 mechi iliyopita ya Ligi Kuu dhidi ya Biashara United, ni wazi Kocha Mkuu, Pablo Franco atahitaji tena kupata ushindi leo ili kujenga morali kwa wachezaji wake kuelekea mechi hiyo dhidi ya Berkane ambao wakiwa nyumbani nchini Morocco kwenye mchezo uliopita walishinda 2-0.

Lakini Pablo atahitaji kuutumia mchezo huo wa leo kama maandalizi kuelekea mechi hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika, ambayo wanahitaji ushindi kwa namna yoyote ile ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu hatua ya robo fainali ya michauno hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Ndiyo, ushindi pekee katika mechi dhidi ya RS Berkane Jumapili, ndio utakaoiwezesha Simba kuendelea kuwa kwenye mstari sahihi wa kufuzu hatua ya robo fainali, hasa ukizingatia baada ya mchezo huo, itakuwa imebakiza mechi mbili moja nyumbani na nyingine ugenini kabla ya kuhitimisha hatua hii ya makundi.

Ikumbukwe katika makundi manne ya michuano hiyo, timu mbili zitakazoshika nafasi ya kwanza na ya pili kwenye kila kundi, zitafuzu moja kwa moja hatua ya robo fainali, na hadi sasa RS Berkane inaongoza Kundi D ikiwa na alama sita, mbili mbele ya Simba na USGN ya Niger zenye pointi nne kila moja huku Asec Mimosas ya Ivory Coasta ikiburuza mkia kwa pointi zake tatu.

Hadi sasa katika kundi hili ndilo linaloonekana kuwa gumu zaidi kwani kila timu ina nafasi ya kuweza kufuzu robo fainali kama ikichanga vema karata zake kwa katika michezo mitatu iliyobaki.

Hata hivyo, kwa kuzingatia ukweli kwamba hakuna timu iliyofanikiwa kushinda ugenini zaidi ya Simba pekee iliyopata sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya USGN, ni wazi kila moja karata yake muhimu ni kuibuka na ushindi nyumbani, hivyo mchezo wa Jumapili si wa kufanya makosa kwa wawakilishi wetu hao.

Kwa namna ratiba ilivyo, Simba na Asec Mimosas katika Kundi D, ndizo zilizobakiza mechi mbili nyumbani, hivyo kinachotakiwa kwa wawakilishi hao wa nchi kimataifa, ni kuhakikisha inapata ushindi katika mechi hizo mbili jambo ambalo litawafanya kufikisha pointi 10, hivyo kuwa na uhakika wa zaidi ya asilimia 70 ya kufuzu robo fainali.

Tuna uhakika viongozi wa Simba, benchi la ufundi na wachezaji, wanajua vema na wana uzoefu mkubwa katika kuzichanga vizuri karata zao kwenye michuano hii hususan wanapocheza katika uwanja wao wa nyumbani, hivyo kilichobaki ni mashabiki kujitokeza kwa wingi katika mechi hizo mbili ili kuipa timu sapoti iweze kuiwakilisha ipasavyo nchi.

Nipashe tunataka kuona kama ambavyo msimu uliopita kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ilivyofanya vizuri na kuiongezea Tanzania pointi hadi kuwa miongoni mwa nchi 12 zilizofikisha pointi za kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo, ikifanya hivyo tena msimu huu wakati huu ikishiriki Kombe la Shirikisho.

Tunaamini kwa aina ya wachezaji Simba ilionao, benchi imara la ufundi pamoja na uongozi uliosimama, ukichagizwa na umoja na mshikamano kutoka kwa mashabiki na wanachama wa klabu hiyo, hilo halitashindikana na kwa mara nyingine tena Tanzania itaingiza timu nne msimu ujao wa michuano hiyo. Katika kufanikisha hilo, Nipashe tunawataka Watanzania wote kuwa kitu kimoja kwa maombi na kuisapoti Simba nje na ndani ya uwanja wakati wawakilishi wetu wa nchi wanapocheza mechi za kimataifa nyumbani na ugenini bila kujali itikadi zetu za kiklabu.

Simba ikishinda Tanzania imeshinda, hivyo tuwe kitu kimoja ili iweze kufika mbali zaidi na kuiongezea nchi pointi zitakazotuwezesha msimu ujao kuingiza timu nne; mbili zitakazokwenda kuwania Ligi ya Mabingwa Afrika na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho.

Lakini lengo letu pia ni kuona bendera ya nchi ikiendelea kupepea vema katika mashindano hayo na kuzidi kulitangaza soka la Tanzania, hivyo Nipashe hatuna budi kuwatakia maandalizi mema na uwakilishi uliotukuka kwenye michuano hiyo kwa kupata ushindi mechi zote zilizosalia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuhama uwanja si suluhisho la tatizo

**MGONJWA** hawezi kupona kwa kuhamishwa kutoka Dar es Salaam na kupelekwa Tabora, ukidhani kuwa eti anaweza kupona kwa kumpeleka sehemu ambayo ugonjwa haukumuanzia huko.

Yeyote atakayefanya hivyo atakuwa anachekesha tu walionuna na hata nia nzuri na mgonjwa. Mgonjwa anatakiwa matibabu tu na kabla ya matibabu, kitachotakiwa ni kufanya vipimo ili kujua nini kinamsibu, kabla ya kupatiwa matibabu, inaweza kuwa dawa, sindano na mengine yanayofanana na hayo.

Kwa siku za karibuni tumeona timu mbili za Prisons na Mbeya Kwanza zimehama uwanja, kwa kile ambacho kinaonekana ni kwamba hazifanyi vizuri kwenye viwanja hivyo. Prisons ambayo misimu miwili ilikuwa inatumia Uwanja wa Nelson Mandela Sumbawanga, imeamua kukimbia na kurejea nyumbani, Sokoine jijini Mbeya.

Ukishangaa ya Musa utaona ya Firauni, siku chache baadaye, timu ya Mbeya Kwanza ambayo ilikuwa inautumia Uwanja wa Sokoine nayo ikatangaza kuhama, yenyewe ikaenda mkoani Ruvuma, ikitangaza kuutumia Uwanja wa Majimaji Songea kama uwanja wao wa nyumbani.

Ina maana wakati Prisons inarejea Sokoine, Mbeya Kwanza nayo ikakimbia uwanja huo.

Wakati viongozi wa Prisons wakiwa hawafichi kuwa wameondoka mkoani Rukwa kwa sababu hawapati matokeo ya kuridhisha, Mbeya Kwanza wao wanadai kuwa ni kupanua wigo wa burudani na kusambaza mchezo huo kwenye mikoa ambayo haina timu za Ligi Kuu.

Mwenyekiti wa Klabu ya Mbeya Kwanza, Mohamed Mashango akadai kuwa mzunguko wa pili, timu hiyo itautumia Uwanja wa Majimaji Songea na kwa kuanzia mechi yao ya Jumamosi dhidi ya Mbeya City ilichezwa uwanjani hapo.

Ukiangalia kwa jicho la tatu, timu hizo zote mbili zinahangaika kwa sababu hazipati matokeo mazuri. Bora Prisons wamejisemea ukweli. Cha kujiuliza, ni kweli viwanja ndivyo vinavyosababisha timu hizi zisishinde na kuamua kuhama?

Je, kuhama ndiyo suluhisho pekee la timu hiyo kuanza kufanya vema kwenye uwanja inayokwenda? Je, viwanja ilivyokuwa ikicheza awali vina mikosi?

Tukianza na Prisons ni kwamba tangu ilipohama Uwanja wa Nelson Mandela na kurejea nyumbani, Uwanja wa Sokoine haijashinda mechi yoyote. Jumatano iliyopita ililazimishwa suluhu kwenye Uwanja wa Sokoine dhidi ya Mtibwa Sugar.

Timu hiyo imeshacheza mechi nne kwenye uwanja huo iliyorejea bila kupata matokeo, tatu zikiwa za Ligi Kuu moja ya Kombe la FA.

Ilichapwa mabao 2-0 dhidi ya Polisi Tanzania, Kombe la FA, ikafungwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, ikalazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City Februari 27, mwaka huu, kabla ya suluhu ya Jumatano.

Prisons haijashinda mechi sita mfululizo za Ligi Kuu moja ya FA, tangu iliposhinda mara ya mwisho bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar Desemba 26, mwaka jana.

Kwa takwimu hizi tu inaonyesaha kuwa Prisons ina tatizo kubwa zaidi na sababu haikuwa Uwanja wa Nelson Mandela. Ama benchi la ufundi ni dhaifu, au wachezaji wake wengi ambao ni maafande wameshakumbwa na umri mkubwa, hivyo yanatakiwa marekebisho makubwa.

Kwa bahati mbaya sana inabidi isubiri msimu ujao na sasa inaburuza mkia kwenye nafasi ya 16 kwa pointi 13.

Mbeya Kwanza nayo, tangu ilipoifunga Kagera Sugar mabao 2-0 Desemba 22, mwaka jana imecheza mechi saba bila kupata ushindi wowote na Jumamosi iliyopita ikicheza kwa mara ya kwanza Majimaji Songea, haikupata ushindi zaidi ya suluhu. Baada ya Prisons kuwa mkiani, timu hiyo ndiyo inafuata, ikiwa nafasi ya 15 kwa pointi 14.

Nayo inaonekana ina matatizo mengine zaidi ya uwanja. Kuhama uwanja imeonekana kama ni staili ya kuficha matatizo yaliyo ndani ya uongozi au timu kwa timu hizo mbili. Inaweza pia kuambukiza hata timu zingine.

Niseme tu viongozi wa klabu hizo watafute chanzo cha timu zao kufanya vibaya ili kurekebisha haraka, vinginevyo zitakuwa na nafasi kubwa ya kushuka daraja msimu huu. Siku zote mficha maradhi mauti humfichua.

## HABARI KITAIFA

# Bunge laridhishwa Barrick mapambano dhidi Ukimwi

**Na Faustine Feliciane**

KAMPUNI ya kuchimba dhahabu kwenye mgodi wa North Mara ya Barrick imetangaza kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa zaidi ya nusu kwa wafanyakazi wake na jamii inayoizunguka kutoka kiwango cha juu cha asilimia 3.3 mwaka 2018 mpaka kufikia asilimia 1.5 mwaka jana.

Aidha, maambukizi mapya ya VVU yamepungua kutoka kiwango cha juu cha asilimia 16 mwaka 2018 na kufikia asilimia 10 mwaka jana.

Akizungumzia mafanikio hayo mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotembelea mgodi huo juzi, kujadili hatua ya kampuni hiyo za kupambana na magonjwa ya maambukizi ya VVU na kifua kikuu, Meneja Mkuu wa mgodi huo, Apolinary Lyambiko, alisema mpango wa VVU na UKIMWI wa kampuni umejikita kuongeza uelewa, kuhimiza ngono salama na kupata ushauri nasaha na upimaji wa hiari (VCTs).

Alisema hilo imesaidia kupunguza kiwango cha magonjwa yote ya zinaa kutoka asilimia 4.78 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 2.95 mwaka jana.

"Katika hili, Barrick ina sera pana kuhusiana na VVU/UKIMWI mahali pa kazi, ambayo imekuwa ikitekelezwa kwa kushirikisha Mganga Mkuu wa wilaya (DMO) na Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), kwenye kampeni zake za kuhamasisha upimaji wa hiari pamoja na kusambaza bure kondomu, kugawa vipeperushi vya kuelimisha na T-shirt, kutoa huduma za uchunguzi wa hali ya afya mara kwa mara, kuboresha mazingira kuhakikisha kuna hewa safi na kufuatilia hali ya usafi katika maeneo ya kazi," alisema Lyambiko.

Vile vile, alisema kwa upande wa jamii, Barrick imeanzisha kampeni mbalimbali za uhamasishaji kwa kushirikiana na DMO ikiwamo kushiriki kikamilifu kwenye maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani.

"Katika kampeni hizo za mwaka 2020 na mwaka jana zaidi ya watu 4,800 walifanya upimaji wa hiari wa afya zao, lakini pia uniti 1,000 za damu zilikusanywa, na kampuni ilitoa vifaa 1,800 vya kupima VVU kwa haraka, watu 164 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi kwa uratibu wa kampuni lakini vipeperushi vingi vya kuelimisha jamii vilitolewa," alisema Lyambiko.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Faustine Ndugulile ambaye ni Mbunge wa Kigamboni, alisema Kamati imeridhishwa na juhudi zinazofanywa kampuni hiyo katika mapambano dhidi ya VVU na Ukimwi pamoja na magonjwa ya zinaa na TB.

"Zaidi tumeridhishwa na utaratibu wa kampuni wa kutowanyanyapaa waathirika wa Ukimwi na TB, waathirika hawa wamekuwa wakiendelea na majukumu ndani ya mgodi kulingana na afya zao, ni jambo zuri na la kujifunza kwa kampuni na taasisi, kamati tunaupongeza sana mgodi wa North Mara na Kampuni ya Barrick kwa ujumla," alisema Ndugulile.

Naibu Waziri wa Madini na Mbunge wa Mbunge wa Longido, Dk. Steven Kiruswa, ameipongeza kampuni hiyo kwa kuwa moja kati ya mbili nchini zilizotambuliwa na mkutano wa kimataifa wa wachimbaji madini uliofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam, kwa vigezo tofauti ikiwamo ubora katika uongozi na utoaji ajira.

## Mwili watelekezwa shamba la mahindi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MWANAMKE ambaye hakutambulika majina yake amekutwa amefariki dunia na mwili wake kutelekezwa kwenye shamba la mahindi.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Katavi, Ali Makame Hamad, tukio hilo lilitokea Mtaa wa Ilembo Manispaa ya Mpanda.

Alisema shamba hilo linamilikiwa na Magdalena Zakayo (40), ambaye ni mkazi wa Makanyagio katika Manispaa hiyo.

Kamanda Hamad alisema mwanamke huyo anakadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 35-40.

Alisema mwili huo haukuweza kutambulika haraka kutokana na kuanza kuharibika.

Alisema mwili huo umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti Hospitali ya Rufani Mkoa wa Katavi kwa ajili ya kusubiri ndugu kuutambua.




Wanawake katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Amina Tindwa (kushoto), wakiwa katika kituo cha kulelea watoto yatima cha Upendo kilichoko Sanangula Manispaa ya Songea kutoa msaada wa vitu mbalimbali kwa kituo hicho wenye thamani ya Sh. 425,000. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# ASBAHAT yaitamani kampeni chanjo ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Wazazi wa Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi, kimesema kinatamani kushiriki katika kampeni ya kuhamasisha chanjo ya UVIKO-19, lakini kinakwamishwa na ukosefu fedha.

Mratibu wa chama hicho taifa, Hidaya Alawi, ndiye aliyesema hayo alipokuwa akizungumza na gazeti hili mkoani Dar es Salaam jana.

Alisema ASBAHAT inatamani kushirikiana na serikali kuharakisha kampeni hiyo ili watu wengi zaidi wajitokeze kuchanja.

"Tunasikia kuwa ni watu 2, 117, 387 tu ndiyo wamechanjwa tangu chanjo ilipoanza kutolewa Agosti mwaka jana, kwa idadi hii ya watu waliochanjwa, ni wazi kwamba kampeni zaidi inahitajika," alisema Alawi.

Alisema ili kuwapo kwa kampeni zaidi, ni vyema serikali ingetenga fungu la fedha na kuwapa wadau mbalimbali wakiwamo ASBAHAT ili nao wafanye kampeni ya uhamasishaji.

"Tunatamani sana kuhamasisha Watanzania kupata chanjo, lakini tunashindwa tuanzie wapi, kwa sababu hatuna fungu la fedha la kutuwezeaha kufanya kazi hiyo," alisema.

Alisema idadi hiyo ya watu waliojitokeza kuchanja inaweza kuwa inasababishwa na elimu potofu ambayo jamii imepata kutoka kwa baadhi ya watu ambao wameamua kufanya upotoshaji.

"Upotoshaji huo unaweza kuisha iwapo wadau wote watashiriki kikamilifu katika utoaji wa elimu sahihi kwa umma na hilo litawezekana kukiwa na fungu maalum la fedha kwa ajili ya kazi hiyo," alisema.

Alisema chama hicho kinatamani kusikia Watanzania wanazungumza lugha moja kuhusu chanjo hasa baada ya umma kupata elimu sahihi kuhusu chanjo na ugonjwa huo. "Tumekuwa tukisikia baadhi ya watu wanadai kuwa hataki chanjo kwa sababu ina madhara au ugonjwa huo haupo, lakini kwa sababu hatuna nyenzo ya kuwezesha kuufikia umma na kuupa elimu sahihi, inabidi tuwe kimya," alisema.

Mratibu huyo alisema, ingekuwa vyema iwapo kila shirika au chama ambacho kiko tayari kuhamasisha au kutoa elimu kuhusu ugonjwa huo kupewa fedha na wataalamu afya na kuzunguka nao katika jamii kuibadili jamii ambayo haijabadilika ili iachane itambue umuhimu wa chanjo.

"Tunatamani tunapotoa elimu kuhusu chanzo cha kuzaa mtoto wa kichwa kikubwa na mgongo wazi, tuelimishe pia kuhusu chanjo na corona. Hili litawezekana iwapo tutakuwa na fedha za kufanya kazi hiyo," alisema.

Alisema, kila Mtanzania kwa nafasi yake anatakiwa kuhamasisha chanjo na kwamba wao, chama njia ya kuwawezesha katika uhamasishaji huo, ni kuwapo kwa fungu la fedha litakalowezesha kuzunguka maeneo mbalimbali.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, akimsikiliza mjasiriamali Angelina Sylivester kwenye maonyesho yaliyoandaliwa na Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake (TWCC) mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wafundwa jinsi ya kuwa viongozi bora

**Mwandishi Wetu**

ASASI ya Wanawake ya Maisha Bora Tanzania (TWBFG) imewafunda wasichana ujasiri wa kuongoza na maisha bora wamalizapo masomo yao, yatatokana na bidii ya masomo na kujitunza kiafya tangu utotoni.

Ushauri huo ulitolewa na TWBFG ilipotembelea Shule ya Msingi Kigezi iliyoko Kata ya Chanika, Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam ili kuelimisha wasichana waliofikia umri wa kupevuka na kuwapa msaada wa taulo za kike.

Elitha Kahembe kutoka katika asasi hiyo alisema wanawake wengi waliopata mafanikio kimaisha kama vile Rais Samia Suluhu Hassan, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, walizingatia maadili na kujibidiisha kielimu tangu utotoni.

"Si mnataka muwe viongozi kama Rais wetu, Samia? Spika wa Bunge?" Basi zingatieni kusoma kwa bidii na kuwa na tabia nzuri kwa kuepuka kudanganywa na vijana ili kufanya mapenzi," aliwaasa.

Kahembe aliwaeleza wasichana hao kuwa wakijihusisha na vitendo vya ngono wakiwa wadogo wanakuwa katika hatari ya kupata mimba za utotoni jambo ambalo linaweza kuzima ndoto za maisha walizojiwekea.

TWBFG walifanya mkutano maalumu na wanafunzi wa kike 241 ambao wamefikia umri wa kupevuka ili kuwaelimisha mambo mbalimbali muhimu kwa maisha yao ya baadaye na namna ya kuhudhuria shule hata nyakati zao za hedhi.

"Tumekuja kuwaelimisha pia namna ya kutumia taulo za kike ili kuepuka kujificha nyumbani unapokuwa katika siku zako za hedhi," alisema Mweka Hazina Msaidizi wa TWBFG, Lydia Maeda.

Wanafunzi hao pia walipewa elimu ya namna ya kuwa wasafi na kuendelea na shughuli zao za kawaida pasipo hofu wawapo kwenye siku zao za hedhi.

Mhazini wa TWBFG, Leonida Lwekamwa, aliwahakikishia wanafunzi hao kuwa asasi yao ipo kwa ajili ya kuwasaidia kwa namna mbalimbali ili wawe wanawake jasiri na wenye maisha bora katika maisha yao.

"TWBFG katika moja ya malengo yake ni kushirikiana na serikali ili kuboresha maisha ya Watanzania kiafya, kielimu, kiuchumi ili kujenga jamii inayoishi maisha bora," alisema Lwekamwa.

Alisema jamii ya Chanika ina bahati kwa sababu TWBFG imelenga kujenga ofisi ya makao makuu katika kata hiyo ya Chanika.

Alisema asasi hiyo imelenga kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa jamii na kuielimisha juu ya kuepuka magonjwa mbalimbali yakiwamo kifua kikuu na maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Naye Elizabeth Kaijage, alieleza majukumu ya TWBFG ni kuyasaidia makundi ya jamii yaliyoko kwenye mazingira magumu kama vile yatima, wajane, jamii inayoishi katika mazingira magumu na kutunza mazingira.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Elimu kwa Umma ya Magonjwa Yasiyoambukiza (TOANCD), Leon Bahati ambaye alikaribishwa kwenye mafunzo hayo aliwatahadharisha kuwa kuna uhusiano kati ya magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyoambukiza.

Pia aliwahadharisha kuacha tabia ya kula vyakula vyenye wingi wa sukari, mafuta na chumvi ili kuepuka magonjwa yasiyoambukiza kama vile matatizo ya meno, shinikizo la damu, kisukari na uzito kupita kiasi.

Wanafunzi hao walieleza changamoto wanazokabiliana nazo kuwa ni uchache wa matundu ya choo, ukosefu wa maji, sehemu za kutupa taulo za kike zilizotumika na baadhi yao hukaa chini madarasani kwa kukosa madawati.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kigezi, Selemani Kyumbo, alisema ofisi yake ina taarifa za changamoto hizo hivyo atajadiliana na TWBFG pmaoja na wafadhili mbalimbali kuona ni namna gani watatatua matatizo hayo.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa shule hiyo, Tutela Lutinaa, alisema shule hiyo itaendelea kushirikiana na TWBFG ili kuendelea kuwakuza kimaadili wanafunzi hao na kuwajengea uwezo wa kujiamini.

# TANROADS yaagizwa ukarabati makaravati

**Na Ibrahim Yassin,**
SONGWE

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, ameuagiza Wakala wa Barabara (TANROADS) mkoa wa Songwe kuhakikisha unasimamia changamoto ya kuziba kwa makaravati katika barabara ya Isongole wilayani Ileje, Kasumulu wilayani Kyela na Ibungu, KK hadi Tukuyu wilayani Rungwe, ili kuondoa adha kwa watumiaji. Barabara hizo ndiyo kiunganishi katika kuzifikia wilaya za Rungwe, Ileje na Kyela ambazo zimetajwa kuwa na changamoto kubwa, hali inayosababisha watumiaji kushindwa kupita kutokana na kupasuka kwa makaravati na kukithiri kwa ubovu wa barabara.

Mhandisi Msongwe ambaye ni Mbunge wa Ileja, alitoa agizo hilo jana wakati wa ziara yake ya kikazi ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo jimboni kwake , ikiwapo barabara zinazosimamiwa na TANROADS na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wilayani humo.

Alisema wananchi wa Tarafa ya Bundali hukumbwa na changamoto ya kutumia barabara hizo kutokana na magari kukwama hususani kipindi hiki cha mvua za masika kutokana na makalavati kujaa maji baada ya kuzibwa na tope, hivyo kuagiza kutatua shida hiyo kwa wakati. "Naagiza meneja wa TANROADS mkoa wa Songwe kufanya ukaguzi wa makaravati yote yaliyozibwa na kuyazibua ili wananchi waendelee kutumia barabara hizo ambazo zimekuwa chachu ya kuwaongezea kipato wananchi kutoka Ileje na wilaya za jirani Kyela na Rungwe sambamba na nchi jirani ya Malawi kupitia boda ya Isongole - Ileje na boda ya Kasumulu - Kyela mkoani Mbeya," alisema Kasekenya.

Akizungumzia kero za barabara hizo Diwani wa Kalembo, Leward Songa, alimwomba Naibu Waziri huyo kuzungumza na TANROADS kutenga mafungu ya kusafisha barabara na kulima barabara kwa mapana ili magari yaweze kupishana na kuepusha ajali zinazosababishwa na uchakavu wa barabara kutokana na majani ya miti kutanda barabarani.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ileje, Ubatizo Songa, alisema licha ya TANROADS kulima barabara kwa kiwango, changamoto iliyoko sasa ni kuziba kwa makaravati.

# NMB yatoa vifaa vya Mil. 29/- Amana Hospitali, Shule 3 Ilala

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Rufaa ya Amana na shule tatu za msingi za Buguruni Kisiwani, Kivule na Airwing zilizoko wilayani Ilala jijini Dar es Salaam, zimeingia katika orodha ya wanufaika wa Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR 2022) ya Benki ya NMB, baada ya Ijumaa iliyopita kukabidhiwa misaada yenye thamani ya Sh. Milioni 29.

Makabidhiano hayo yalifanyika Shule ya Msingi Buguruni Kisiwani, ambako Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Ilala (DC), Ng'wilabuzu Ludigija, vifaa vyenye thamani hiyo, ambayo ni kati ya Sh. Bilioni 2.8 zilizotengwa na benki hiyo kusaidia Sekta za Elimu na Afya kwa mwaka 2022.

Wakati Hospitali ya Amana ikikabidhiwa masanduku ya kuhifadhia vifaa tiba vya wagonjwa waliolazwa 'bed side rockers' 30 zenye thamani ya Sh. Mil. 9.2, Shule ya Airwing ilikabidhiwa madawati 100 yenye thamani ya Sh. Mil. 10, huku Shule ya Buguruni Kisiwani ikikabidhiwa mabati 150 yenye thamani ya Sh. Mil.4.8.

Nayo Shule ya Msingi Kivule, ilikabidhiwa madawati 50 yenye thamani ya Sh. Mil. 5, hivyo kufanya jumla kuu ya thamani kufikia Sh. Mil. 29, ambako DC Ludigija aliishukuru benki hiyo na kusema anaamini misaada hiyo inaenda kuamsha ari ya kujisomea na kuboresha mazingira ya kufundishia, pamoja na kuhudumia wagonjwa.

Ludigija aliitaka Benki ya NMB kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, katika kunyanyua elimu na kuboresha miundombinu ya afya wilayani mwake, ambako uwingi wa shule na hospitali, umesababisha kuongezeka kwa wanafunzi na wagonjwa, hivyo kuongeza changamoto.

"Serikali tunawashukuruni kwa namna mnavyojitoa kutatua changamoto kwenye elimu na afya wilayani Ilala, ambako uhitaji ni mkubwa na bado nguvu ya Serikali haitoshi bila sapoti za wadau.

Kwa hili mnadhihirisha ukweli kuwa; 'Ninyi NMB ni Benki Baba Lao,' mnaoongoza katika kutekeleza takwa la CSR," alisema Ludigija.

Kwa upande wake, Donatus aliishukuru Manispaa ya Ilala pamoja na viongozi wa shule zilizokabidhiwa misaada hiyo kwa kuitazama NMB kama mshirika sahihi katika utatuzi wa changamoto, hivyo kuipelekea maombi yao na kwamba wao wanajisikia faraja kuwa wadau vinara katika kurejesha kwa jamii sehemu ya faida yao.

"Misaada hii tunaitoa chini ya mwamvuli wa CSR, programu ya kila mwaka, ambayo kwa mwaka huu wa 2022 tumetenga kiasi cha Sh. Bilioni 2.8 ambazo ni sawa na asilimia 1 ya faida yetu kwa mwaka uliopita, tukirejesha kwa jamii, ambayo ndio sehemu ya wateja wetu.

"Kwa sababu sehemu ya faida tunairudisha kwao, basi wito wetu wa Watanzania ni kutumia huduma zetu zilizotapakaa matawini kote nchini, ambako kuna mikopo ya riba nafuu kwa kada zote za wafanyakazi, wakulima, wafanyabiashara, wajasiriamali, wafugaji na wavuvi. NMB ndio suluhu ya changamoto za kifedha," alisisitiza Donatus.

Akisoma risala ya shule kwa Mkuu wa Wilaya, Mwalimu Lilian Saguti wa Shule ya Buguruni Kisiwani, alisema shule hiyo iliyoanzishwa miaka 19 iliyopita (2003), kwa sasa ina wanafunzi 1169 na walimu 32, huku ikikabiliwa na changamoto za madawati, viti na meza za walimu, pamoja na vifaa vya michezo, ikiwemo viwanja.

# Wanawake wajasiriamali wairidhisha serikali

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeridhishwa na hatua ya wanawake wengi wajasiriamali wanaoshiriki Maonyesho ya Pili ya Bidhaa za Wanawake Wajasiriamali kutoka maeneo mbalimbali ya nchi kuwa na bidhaa zenye viwango, hivyo kuwa fursa nzuri ya kuimarisha uchumi wa familia zao. Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Seleman Jafo, wakati akifungua Maonyesho ya Pili ya Bidhaa za Wanawake Wajasiriamali yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Jafo, alilipongeza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa kazi nzuri na kulitaka shirika hilo kusaidia vikundi vya kinamama ili viweze kuratibiwa vizuri.

Alisema baadhi ya wanawake wana changamoto mbalimbali na wengine hawajapata alama ya ubora ya TBS, hivyo alitoa wito kwa wadau wote wanaoshughulika na wanawake wajasiriamali kuhakikisha wanaondoa vikwazo kwa kinamama hao ili waweze kusonga mbele.

"Kwa nilichokiona sasa naamini sasa mpo vizuri na hii ina maana kwamba wanawake wakijenga uchumi watasababisha kuimarisha familia zao na hivyo kuwa na maisha bora zaidi," alifafanua Jafo.

Awali akizungumza na waandishi wa habari Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS, Amiti Msanjila, alisema wameshiriki maonyesho hayo kutokana na wao kuwa wadau wakubwa katika kuwezesha biashara kwa lengo la kuwapatia elimu washiriki kuhusiana na namna ya kupata alama ya ubora, usajili wa bidhaa za vipodozi pamoja na vyakula.

Alisema TBS imekuwa ikitoa alama ya ubora kwa wajasiriamali bure, hivyo ili waweze kuhudumiwa na shirika hilo wanatakiwa kuwa na barua ya utambulisho kutoka SIDO na mtaji wao uwe chini ya milioni 70.

"SIDO wanatuandikia barua kuwatambulisha kwetu huwa huyu ni mjasiriamali mdogo na akishaleta hiyo barua tunamhudumia bure kuanzia gharama ya upimaji," alisema Msanjila.

Kuhusu faida ya alama ya ubora kwa bidhaa, Mjanjila alisema inaongoze imani kwa umma kwamba bidhaa zao ni salama na zinakidhi matakwa ya viwango, hivyo zinaweza kufanyakazi iliyokusudiwa.

Aliongeza kwamba alama ya ubora inawawezesha wazalishaji bidhaa zao kukubalika sokoni kwa sababu tayari zimethibitishwa ubora wake na hivyo kuwa na uwezo wa kuhimili ushindani.

Kwa upande wake Meneja wa Mawasiliano ya Umma na Masoko wa TBS, Gladness Kaseka, alisema maonyesho hayo ni fursa nzuri kwa shirika hilo kukutana na washiriki 400 na kufikisha ujumbe kuhusiana na mpango wa shirika kuthibitisha bure bidhaa za wajasiriamali. Alifafanua kwamba kila mwaka serikali inatenga zaidi ya Sh. milioni 200 kuhudumia wajasiriamali wadogo, hivyo kupitia maonyesha hayo wameweza kupata fursa ya kuzungumza nao, kuwatembelea kwenye mabanda yao kusikiliza changamoto zao na kuwaelekeza hatua ambazo wanaweza kuchukua kuzipatia ufumbuzi.

Alitoa wito kwa wanawake wajasiriamali kuchangamkia fursa hiyo kwa sababu hakuna anayejua kesho itakuwaje, kwa sababu sasa hivi huduma hiyo inatolewa bure ili mradi wawe na barua ya utambulisho kutoka SIDO.

Maonyesho hayo yalioanza Machi 3, mwaka huu, yaliandaliwa na Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania Tanzania (TWCC) na yanatarajiwa kumalizika kesho.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Pwani na Zanzibar, Donatus Richard, akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi mabati na madawati kwa Shule za Msingi za Airwing, Kivule na Buguruni Kisiwani pamoja na kabati za kuhifadhia dawa katika Hospitali ya Rufani ya Amana, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 29. Wapili kutoka kulia (mbele) ni Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'walabuzu Ludigija, Meya wa Jiji la Ilala, Said Kumbilamoto, na Meneja wa NMB Tawi la Ilala, Christine Ufiga (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wagonjwa wa figo kupunguziwa gharama

**Na Yasmine Protace**

SERIKALI imeanza kuchukua hatua kupunguza gharama za kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo.

Kwa sasa inatumia zaidi ya shilingi bilioni 29 kufanya huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo 1,000 nchini kwa mwaka.

Hayo yalibainishwa na Mdhibiti Ubora kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) Joseph Kitukulu, wakati akizungumza katika warsha ya wanahabari iliyokuwa ikizungumzia mikakati ya kupambana na ugonjwa wa figo.

"serikali inatumia zaidi ya shilingi bilioni 29.484 kwa mwaka kufanya huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa 1,000," alisema.

Katukulu alisema MSD itaokoa zaidi ya shilingi bilioni 13, hivyo kuboresha upatikanaji wa huduma zinazoambatana na hiyo.

Mratibu wa figo kutoka Wizara ya Afya, Dk. Linda Ezekiel, alisema kuwa mgonjwa mmoja ambaye anasafisha figo hutumia zaidi ya shilingi milioni 40 kusafisha figo nchini kwa mwaka.

Dk. Linda alisema maradhi ya sukari na shinikizo la juu la damu husababisha watu kuugua ugonjwa wa figo.

Aliongeza kuwa mtindo wa maisha usiozingatia ulaji wa lishe nao huchangia watu kupata ugonjwa wa figo sugu, ambapo mtu anapoanza kusafisha figo anatumia fedha nyingi.

Aliongeza kuwa katika kukabiliana na matumizi makubwa ya kusafisha figo, MSD imeagiza mashine za kusafisha damu kutoka kwa watengenezaji ili kuwezesha upatikaji wa huduma hiyo kwa gharama nafuu na rahisi kwa wagonjwa wa figo nchini.

Aliesema ili kuwapunguzia wagonjwa gharama, serikali imeagiza mashine 171 za kusafisha damu na mashine za kuchakata maji 11.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja wa awamu ya sita, serikali imewekeza zaidi ya shilingi bilioni moja katika huduma za usafishaji damu zipatikane katika hospitali zote nchini.

# Kampeni kurejesha uoto wa asili yaanza

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imezindua kampeni ya upandaji miti maeneo ya pembezoni mwa vyanzo vya maji, shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu ambayo ni hatua ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni hatua ya kurejesha uoto wa asili.

Uzinduzi wa kampeni hiyo umeanza katika Shule ya Sekondari SUA, na Mbuyuni ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa lengo lililowekwa na Manispaa hiyo ya kupanda miti milioni 1.5 .

Akizungumza katika uzinduzi huo, Ofisa Mazingira Manispaa ya Morogoro, Samwel Subby, alisema juzi mjini hapo kuwa lengo la kampeni hiyo yenye kauli mbiu ya "Soma na mti" ni kuhakikisha wanafunzi waone upandaji miti ni sehemu ya maisha ili kukabili changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

"Tumeanza kampeni hii kwenye Shule ya Sekondari Mbuyuni na SUA, tunawashukuru wadau wetu Shirika lisilo la kiserikali la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT) kwa kutupatia miche 1,000 ambayo tumeipanda," alisema Subby.

Alisema ili kampeni hii iweze kufanikiwa, ni muhimu kwa kila mwanafunzi kupanda mti mmoja na autunze hadi anapomaliza shule sambamba na taasisi zipande miti kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Subby aliagiza kwa viongozi wa shule za msingi na sekondari kufufuliwa kwa klabu za utunzaji wa mazingira katika shule ambazo zisimamiwe na maofisa elimu kwa vitendo ili kampeni ya soma na mti kuhakikisha inatekelezwa kikamilifu.

Aliwapongeza viongozi wa kata, vyama vya siasa, wananchi na wadau wote wa mazingira wakiwamo wanafunzi kushiriki katika kampeni hiyo.

Naye Diwani wa Kata ya Mbuyuni, Samwel Msuya, aliushukuru uongozi wa manispaa hiyo na wadau wengine kuzindua kampeni hiyo katika kata hiyo na kuwashauri wenye viwanja vipya kupanda miti mitatu katika viwanja vyao.

Mwanafunzi wa kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Mbuyuni, Elizabeth Ngonyani, aliiomba jamii na wanafunzi kusimamia kampeni hiyo ili ifanikiwe sambamba na kwa serikali kuwachimbia kisima ili kurahisisha upatikanaji wa maji ya kutunza miti inayopandwa.

# Mradi kuhimili mabadiliko ya tabianchi waja

**Na Mwandishi Wetu,** BUNDA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limezindua Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Wilaya ya Bunda mkoani Mara.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo uliofanyika jana wilayani hapo, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Menan Jangu, alisema lengo la mradi ni kutekeleza shughuli zitakazosaidia kuhimili athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi katika sekta za uvuvi, mazingira, maji na kilimo.

Alisema katika sekta ya uvuvi mradi utasaidia kuhakikisha uvuvi unakuwa endelevu kwa kuzuia uvuvi haramu, kuongeza mazalia ya samaki pamoja na ufugaji wa samaki wa kisasa kwa njia ya vizimba.

Kwa upande wa kilimo, alisema mradi utasaidia kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji kwa mazao ya chakula kama vile mpunga pamoja na mboga, pia mazao yanayostahimili ukame kama vile mihogo, choroko pamoja na alizeti.

Alitaja lengo lingine la mradi ni kuhakikisha mnyororo wa thamani unakamilika ikiwa ni pamoja na kujenga maghala, mashine za kukoboa, kukamua na kukausha mazao.

Mratibu wa Mfuko wa Adaptation Fund, unaofadhili mradi huo, Fredrick Mulinda, aliipongeza Halmashauri ya Bunda kwa kuwa miongoni mwa wanufaika wa miradi minne ya kwanza, mingine ikiwa wilaya za Kongwa, Nyanda kame za kati Dodoma, Singida, Tabora, Zanzibar na Bunda.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Joshua Nasari, aliwapongeza wataalamu wa Halmashauri ya Bunda pamoja na NEMC kwa kuandika andiko zuri ambalo limesaidia kupatikana kwa fedha zitakazohudumia kata nane katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mshauri Mwelekezi wa Mradi, Dk. Masinde Bwire, alisema malengo mengine ya mradi ni kupunguza ukame kwa kuongeza upandaji wa miti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Prof. Esnat Chaggu, aliipongeza Halmashauri ya Bunda kwa kuwa ya kwanza Tanzania kupokea fedha kupitia mfuko wa mabadiliko ya tabianchi na aliwaomba wahakikishe wanatumia fedha kama andiko lilivyoidhinisha na siyo tofauti kwa maendeleo endelevu. •




Wanafunzi wa kike kutoka shule mbalimbali za sekondari nchini wakionyesha jinsi ya kutengeneza tovuti baada ya kupata mafunzo ya TEHAMA kupitia mpango wa 'Code like a girl' wenye kuwezesha wasichana kujifunza bunifu mbalimbali yaliyoandaliwa na Taasisi ya dLab na kudhaminiwa na Vodacom Tanzania Plc, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ridhiwani ataja suluhisho migogoro ardhi

**Na Julieth Mkreri,** CHALINZE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amesema ili kuondokana na migogoro ya ardhi ni vema kila mwananchi ahakikishe ana hati miliki ya eneo lake.

Ridhiwani aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wananchi wa vijiji vya Kwamsanja, Kwamduma na Kwakonje ambapo walimwelezea kuhusiana na migogoro isiyoisha inayosababisha kutokuwa na maendeleo.

Alisema kero ya migogoro ya ardhi imekuwa ikielezewa na wananchi katika maeneo mbalimbali aliyopita na mwarobaini wa tatizo hilo ni kuwa na hati miliki ambayo itakuwa inaelezea mipaka ya kila mmoja pamoja na vijiji.

"Wenyeviti hakikisheni wananchi wanapimiwa maeneo wakuwa na hati miliki ili kuondoa hii migogoro ya mara kwa mara, simamieni pia vijiji vyenu vihakikiwe mipaka yake itasaidia kufanya shughuli nyingine za maendeleo badala ya kila siku kufanya usuluhishi," alisema.

Kuhusiana na suala la mifugo kuharibu mazao ya wakulima, Ridhiwani aliwataka watendaji kusimamia sheria ndogo zinazotungwa na Baraza la Madiwani ili kukomesha hali hiyo.

Ofisa Ardhi wa Halmashauri ya Chalinze, Musa Kichumu, aliahidi kushughulikia maagizo ya Naibu Waziri huyo, huku akiwataka wananchi kuheshimu mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao kila mmoja ametengewa eneo lake kwa jamii ya wafugaji na wakulima.

Aidha, alieleza kuwa ipo haja ya elimu kwa wananchi kuhusiana na mpango wa matumizi bora ya ardhi ili wasisitizwe kuzingatia mipango hiyo kuepuka migogoro ya mara kwa mara.

Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Chalinze, Msongo Songoro, alisema ipo sheria imepitishwa na madiwani kuondoa na kusubiri Waziri wa TAMISEMI kusaini na itakapoanza kila ng'ombe atakayekutwa kwenye eneo ambalo haliruhusiwi kisheria atatozwa Sh. 50,000.

Songoro alisema sheria hiyo ni kati ya zilizotungwa na halmashauri kuondoa migogoro kwenye baadhi ya maeneo ya halmashauri hiyo mingi ikihusishwa wafugaji wanaolalamikiwa kusha mifugo kwenye mashamba ya wakulima.

Wakizungumza katika mikutano tofauti iliyofanywa na Ridhiwani ambaye ni Mbunge wa Chalinze, walimweleza kuwa wanashindwa kufanya shughuli za maendeleo kutokana na muda mwingi kutumia wakisuluhisha migogoro.

Ramadhani Mtui na Juma Chambila wakazi wa Kibindu walieleza kuwa kwenye baadhi ya mashamba yao wanashindwa kuendesha shughuli za kilimo kutokana na jamii ya wafugaji kulisha mifugo kwenye mashamba yao.

Mtui aliiomba serikali kuingilia kati kwani kuna hatari ya kukumbwa na baa la njaa kwa jamii ya wakulima endapo hakutakuwa na udhibiti wa mifugo kwenye maeneo ya kilimo.

# Wakulima wazawa wahakikishiwa soko

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wazawa wamehakikishiwa uhakika wa masoko ya mazao yao.

Hatua hiyo imetokana na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kusema itaendelea na utaratibu wake wa kununua malighafi zinazotumika kutengenezea bia zake kutoka kwa wakulima wa ndani pamoja na kuwaingiza wakulima wengi zaidi katika mpango wake huo.

Kwa sasa SBL inanunua malighafi kutoka kwa mtandao wa wakulima zaidi ya 400 waliopo sehemu mbalimbali nchini ambao wanaiuzia kampuni hiyo zaidi ya asilimia 70 ya malighafi inazohitaji kwa mwaka kwa ajili ya uzalishaji wa bia.

Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, alisema kupitia mpango wake wa kilimo biashara SBL inawahakikishia wakulima wazawa soko ka uhakika wa mazao kama shayiri, mtama na mahindi ambayo hutumia kutengenezea bidhaa zinazotengenezwa kwa viwanda vyake vilivyoko Dar es Salaam, Moshi na Mwanza. "Wakulima wengi wananufaika kutokana na mradi huu kwa kuwa tunawapa soko la uhakika. Pamoja na soko la uhakika, tunawapatia mbegu bora bure, tunawaunganisha na taasisi za kifedha kwa ajili ya kupata mitaji ya kupanua uzalishaji wao na pia tunawapatia mbolea na pembejeo nyingine za kilimo," alisema Wanyancha.

Wanyancha aliongeza: "Wakulima wengi walio chini ya mpango huu wameweza kukua kwa maana ya kuongeza uzalishaji na pia kuboresha hali zao za kiuchumi. Tatizo kubwa la wakulima hawa lilikuwa soko la uhakika na namna ya kupata mitaji ya kuongeza uzalishaji wao na utaratibu wa kuwaunganisha na taasisi za kifedha umeleta mafanikio makubwa katika shughuli zao."

Wakizungumza na gazeti hili baadhi ya wakulima walisema mpango huo umewasaidia kulima kisasa huku ukiwahakikishia soko kwa mazao kama shayiri, uwele pamoja na mahindi ambayo huiuzia SBL

Mwinyi Makame, kutoa wilayani Hanang mkoani Manyara anayenufaika alisema mradi huu umefungua milango ya mafanikio katika shughuli zake za kilimo, na kuwa SBL imekuwa ikimpatia pembejeo muhimu za kilimo kama mbegu, mbolea, dawa za wadudu jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limesaidia kuongeza uzalishaji wangu tofauti na siku za nyuma.

Bora Msaki mkulima mwingine anayenufaika na mpango huo ambaye alianza na ekari 50 na ambaye kwa sasa analima zaidi ya ekari 200 za shayiri eneo la West Kilimanjaro mkoani Kilimanjaro, alisema maisha yake yamebadilika sana baada ya kuingia katika mpango huo na kwamba wamepewa elimu ya kilimo cha kisasa pamoja na msaada wa huduma za kighani.

Nipashe
Spotika



MATAJIRI WA5 WANAOTAKA KUINUNUA CHELSEA FC 21 UK. 12-13



# NYOTA WA5 WA THAMANI ZAIDI WA MINO RAIOLA

**LONDON,** England

MINO Raiola ni jina ambalo limezoeleka sana kwa mashabiki wa soka. Ni wakala wa wachezaji akiwakilisha idadi kubwa ya wanasoka wa kiwango cha juu. Licha ya kuwa mtu wa mgawanyiko katika ulimwengu wa kandanda, Raiola anatoa huduma nzuri kwa wateja wake na ni mzuri sana linapokuja suala la mikataba yenye faida kwao.

Wakala huyo wa hali ya juu anajulikana kwa kutangaza habari kwa kauli zake za ajabu, hasa kwa heshima na wateja wake wa kiwango cha juu. Kwa mfano, aliidhalilisha hadharani klabu ya mteja wake, Paul Pogba ya Manchester United mara kadhaa.

Raiola anafanya hivi ili kushawishi maoni ya umma na kuongeza shinikizo kwa klabu ili wachezaji anaowawakilisha wapate wanavyotaka.

Makala haya tunawaangalia wateja watano wa thamani zaidi wa Mino Raiola, haya sasa...

**#5. MARCO VERRATTI (PARIS SAINT-GERMAIN) - EURO MILIONI 55**

Marco Verratti ni mmoja wa viungo bora zaidi duniani. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia alichangia kwa kiasi kikubwa mbio za ushindi za Italia kwenye Euro 2020. Verratti ni kiungo wa kati ambaye ni mwepesi sana na ni bora akiwa na mpira miguuni mwake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, pia ni mpiga pasi mzuri sana wa mpira na anaweza kuimarisha ulinzi kwa usahihi wake na kwa ukali kupitia mipira. Verratti kwa sasa amesaini PSG kwa mkataba unaomweka hadi mwaka 2024. Amekuwa na wababe hao wa Ligue 1 tangu mwaka 2012 na ni mmoja wa wachezaji wao muhimu.

Muitaliano huyo amekuwa akipata majeraha ya mara kwa mara na hilo limekuwa likimzuia Verratti kuongeza uwezo wake. Lakini akiwa kwenye kiwango chake, hawezi kuzuilika.

**#4. PAUL POGBA (MANCHESTER UNITED) - EURO MILIONI 55**

Mino Raiola ameingia kwenye vichwa vya habari kwa kuzungumzia mustakabali wa Paul Pogba mara kadhaa katika siku za hivi karibuni. Ni salama kusema kwamba hana mashabiki katika nusu ya Manchester, haswa baada ya kuidhoofisha klabu na maoni yake Desemba 2020.

Licha ya maoni hayo, Pogba anaendelea kubakia Manchester United, lakini anatarajiwa kuwa mchezaji huru msimu huu wa majira ya joto. Mfaransa huyo ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani, lakini kwa sasa mustakabali wake bado haujatatuliwa.

Haijabainika iwapo Raiola atatafuta ofa ya mkataba mpya kutoka kwa United kwa ajili ya mteja wake au kama anatafutiwa makazi mapya.

Katika mechi 19 katika michuano yote kwa Man United msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, amefunga bao moja na kutoa asisti nane.

**#3. GIANLUIGI DONNARUMMA (PARIS SAINT-GERMAIN) - EURO MILIONI 65**

Gianluigi Donnarumma alichomoza kwenye ulimwengu wa soka akiwa na umri wa miaka 16. Alikaa miaka sita kule AC Milan kabla ya kuwaacha kama mchezaji huru msimu uliopita na kujiunga na PSG. Donnarumma alitoa mchango mkubwa Italia ikishinda Euro 2020 mwaka 2021.

Aliwaongoza kupata ushindi mfululizo wa mikwaju ya penalti katika nusu fainali ya mashindano hayo na akatajwa kuwa mchezaji bora wa michuano hiyo. Donnarumma hajaweza kuwa na mechi nyingi za kuanza PSG. Amelazimika kupishana na Keylor Navas, bado kipa mwingine wa kiwango cha dunia.

Donnarumma ni mmoja wa wachezaji wa thamani zaidi wanaowakilishwa na wakala bora Raiola. Thamani yake ya soko la uhamisho inasimama kwa euro milioni 65.

**#2. MATTHIJS DE LIGT (JUVENTUS) - EURO MILIONI 65**

Matthijs De Ligt alikuwa nahodha wa Ajax na kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19 kabla ya kuhamia Juventus mwishoni mwa msimu huo. Maisha ya De Ligt yamedumaa kidogo tangu wakati huo, lakini hakuna shaka juu ya uwezo wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

Baada ya kutokuwa na nafasi mbele ya Leonardo Bonucci na Georgio Chiellini katika misimu yake miwili ya kwanza, De Ligt sasa amekuwa tegemeo katika kikosi cha kwanza cha Bianconeri hao msimu huu. Ni mchezaji aliyeimarika zaidi msimu huu na kwa mara nyingine tena anavutia hisia kutoka klabu nyingine za Ulaya.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2024, lakini Juventus imeripotiwa kumtaka aongeze muda mfupi. Hii ni ili waweze kumuuza kwa kiasi kikubwa cha fedha mwishoni mwa msimu wa 2022-23.

**#1. ERLING HAALAND (BORUSSIA DORTMUND) - EURO MILIONI 150**

Erling Haaland tayari amejitambulisha kama mmoja wa washambuliaji bora zaidi barani Ulaya katika misimu michache iliyopita. Ana umri wa miaka 21 pekee, lakini ni mmoja wa washambuliaji wanaosakwa sana kwa sasa.

Haaland anakaribia kuondoka Borussia Dortmund msimu wa majira ya joto unaokuja wakati kifungu cha kutolewa cha euro milioni 70 katika mkataba wake kitakapoanza kutumika. Wakala wake, Raiola tayari amezunguka huku na huko akiwatembelea wababe kadhaa wa Ulaya kufanya majadiliano juu ya mpango unaowezekana.

Tangu ajiunge na kikosi hicho cha Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga Januari 2020, Haaland amefunga mabao 80 na kutoa asisti 21 za mechi 78 katika mashindano yote. Licha ya kuwa mchezaji mdogo zaidi kwenye orodha, Haaland ndiye mteja wa thamani zaidi wa Raiola.

## ISIKUPITE

CARLOS Vela wa Los Angeles FC, ndiye mchezaji wa soka anayeingiza kiasi kikubwa cha fedha kwa mwaka kwenye Ligi Kuu Marekani (MLS), akikunja dola milioni 6.3 akifuatiwa na Javier 'Chicharito' Hernandez (LA Galaxy) dola milioni sita huku Gonzalo Higuain wa Inter Miami akishika nafasi ya tatu kwa kuvuta dola milioni 5.79.



## Extra Time

# MATAJIRI WA5 WANAOTAKA KUINUNUA CHELSEA FC

**LONDON,** England

MMILIKI wa Klabu ya Chelsea, Roman Abramovich, amefanya maamuzi ya kuiuza klabu hiyo baada ya sakata la Urusi kuishambulia Ukraine hali iliyotishia kutaifishwa kwa mali zake nchini England.

**Anatajwa kwamba ni mmoja wa watu wa karibu sana wa Rais wa Urusi, Vladimir Putin na hivyo kuwekewa vikwazo vya kibiashara kwa sababu ya vita inayoendelea nchini Ukraine.**

Katika ujumbe uliotumwa katika tovuti ya klabu hiyo, Abramovich aliweka wazi kuwa yamekuwa maamuzi magumu kwake, lakini amefanya hayo yote kwa ajili ya kulinda heshima ya klabu hiyo.

"Ningependa kushughulikia uvumi katika vyombo vya habari katika siku chache zilizopita kuhusiana na umiliki wangu wa Chelsea FC.

"Kama nilivyosema hapo awali, kila mara nimekuwa nikichukua maamuzi kwa nia njema ya klabu.

"Kwa hali ilivyo sasa, nimechukua uamuzi wa kuiuza klabu, kwani naamini hii ni kwa manufaa ya klabu, mashabiki, wafanyakazi, pamoja na wadhamini na washirika wa klabu.

"Uuzaji wa klabu hautaharakishwa bali utafuata taratibu zinazostahili. Sitaomba mkopo wowote ulipwe. Hii haijawahi kuwa kuhusu biashara wala pesa kwangu, lakini kuhusu mapenzi safi kwa mchezo na klabu.

"Zaidi ya hayo, nimeiagiza timu yangu kuanzisha msingi wa hisani ambapo mapato yote kutokana na mauzo yatachangwa.

"Msingi huo utakuwa kwa manufaa ya waathiriwa wote wa vita nchini Ukraine. Hii ni pamoja na kutoa fedha muhimu kwa mahitaji ya dharura na ya haraka ya waathiriwa, pamoja na kusaidia kazi ya muda mrefu ya kurejesha.

"Tafadhali fahamu kuwa huu umekuwa uamuzi mgumu sana kufanya, na inaniuma sana kuachana na klabu kwa njia hii. Hata hivyo, ninaamini hii ni kwa manufaa ya klabu."

Baada ya tangazo hilo mabilionea kadhaa duniani wamejitokeza hadharani kuingia kwenye kinyang'anyiro cha kuinunua klabu hiyo.

Abramovich ambaye alijiuzulu nafasi ya kuwa ndani ya uongozi wa bodi na kubaki kuwa mmiliki, alikuwa na timu hiyo tangu mwaka 2003.

Bei iliyotajwa na Abromovich ni pauni bilioni tatu. Aliinunua Chelsea mwaka 2003 kwa pauni milioni 140.

Hapa tunawaangalia mabilionea waliotangaza nia ya kutaka kuinunua klabu hiyo ambayo imekuwa na mafanikio makubwa kwenye Ligi Kuu England tangu kuchukuliwa na Abromavich.

Imetwaa taji la Ligi Kuu mara tano, FA mara nne, Ngao ya Jamii mara mbili, pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili, twende sasa...

### #1. LOUFTY MANSOUR

Bilionea wa Misri, Loufty Mansour mwenye umri wa miaka 33, ameonyesha nia ya kuinunua Chelsea yenye maskani yake pale Stamford Bridge. Loufty ni mtoto wa kiume wa bilionea wa Misri, Mohamed Mansour.

Pia Loufty ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Man Capital inayojihusisha na uwekezaji na inayomilikiwa na Kampuni mama ya Mansour Group.

Katika jambo linaloonyesha upenzi wake kwa Chelsea, Mansour ana tiketi ya msimu mzima kwa mechi zote za uwanja wao wa nyumbani, Stamford Bridge.

Anatajwa kwamba anamiliki utajiri wa thamani ya dola bilioni 11.

### #2. HANSJORG WYSS

Bilionea Hansjorg Wyss ni raia wa Uswisi na inaelezwa kuwa yupo kwenye hesabu za kuhitaji kuwa mmiliki wa Chelsea kwa kuwa anahitaji kuinunua baada ya Abramovich kuiweka sokoni.

Bilionea huyo mwenye miaka 86, inaonekana kwamba anauhitaji umiliki wa Chelsea inayotumia Uwanja wa Stamford Bridge.

Yeye ni Rais na Mwenyekiti wa Kampuni ya Synthes Holding AG iliyoko nchini Marekani inayozalisha vifaa tiba. Baada ya tangazo la Chelsea kuwekwa sokoni, Wyss alinukuliwa na gazeti la Blick akisema:

"Abramovich anajaribu kuweza kuuza vitu vyake vyote vya gharama ambavyo vipo England, pia anataka kufanya hivyo katika suala la Chelsea haraka."

"Mimi nimepokea ofa ya kuinunua Chelsea kutoka kwa Abramovich, ninapaswa kusubiri sasa kwa muda wa siku nne ama tano kuanzia sasa, kwa kuwa tumeipata ofa hiyo Jumanne, lakini Abramovich kwa sasa anahitaji fedha nyingi.

"Kwa namna yoyote ile atahitajika kupunguza kiasi cha fedha anachokitaka, kwa sababu ni kikubwa sana."

Bilionea huyo anatajwa kuwa na utajiri wa pauni bilioni 5.1.

### #3. CONOR MCGREGOR

Huyu ni mwanamichezo ambaye ni mchezaji wa ngumu na mateke (kick boxing) na 'mixed martial artist' mwenye umri wa miaka 33.

Anatajwa kwamba, kwa mwaka anaingiza dola milioni 180. Naye amejitokeza hadharani kutangaza kwamba anataka kuinunua Chelsea.

Mara baada ya Abramovich kutangaza kuiuza klabu hiyo, McGregor aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter:

"Chelsea inauzwa pauni bilioni tatu. Ngoja nikainunue haraka inavyowezekana."

Hata hivyo, utajiri wake haujawekwa hadharani na wengi wanaamini kuwa hana fedha za kutosha kuinunua klabu hiyo.

### #4. SIR JIM RATCLIFFE

Huyu licha ya kwamba ni shabiki mkubwa wa Manchester United, lakini naye ana tiketi ya msimu kuishuhudia Chelsea kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Stamford Bridge.

Ratcliffe pia ana miliki klabu ya soka ya Nice ya nchini Ufaransa. Kwa mara ya kwanza alijaribu kutaka kuinunua Chelsea mwaka 2019.

Anatajwa kwamba ana utajiri wa pauni bilioni 20 akiwa ana miliki kampuni kubwa ya kemikali ya Ineos.

Bilionea huyo mwenye umri wa miaka 69, amebainisha kwamba amefanya mazungumzo binafsi na Abromavich kuhusu kuinunua klabu hiyo.

### #5. TODD BOEHLY

Baada ya kujaribu kuinunua Chelsea mwaka 2019, bilionea huyu wa Marekani, Boehly sasa anaweza kutimiza ndoto zake.

Bilionea huyu ni shabiki mkubwa sana wa michezo na alitoa ofa mbili mwaka 2029 kwa ajili ya kuinunua klabu hiyo.

Boehly ni mwanzilishi, Mwenyekiti na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Eldridge Industries na utajiri wake unatajwa kuwa pauni bilioni 4.72.

Eldridge ni kampuni yenye ofisi katika majiji ya London (England), New York na Boston (Marekani).



LOUFTY MANSOUR

## Nukuu

"Kwa mashabiki wengi wa Man United, wataumia sana kumtazama [Cristiano] Ronaldo kwa sasa. Ana miaka 37; amewapita wanasoka wengi kwa miaka mitano au sita, lakini huwezi kujificha kutokana na kuzeeka. Umri unamfika kila mtu, na inaonekana umemfika Ronaldo. Miguu yake inaonekana kuchoka; haonekani kuwa mwepesi na mkali katika kuwazunguka wachezaji wa pande zote," **Mshambuliaji wa zamani wa Aston Villa, Gabriel Agbonlahor**



"Hawa wawili [Chelsea na Liverpool] hawatakuwa maili milioni moja. Wamepata safu mbili bora za ulinzi barani Ulaya na kama unataka kushinda (Ligi ya Mabingwa) soka ni kwa miguu miwili, unahitaji kutoruhusu bao. Wako vizuri sana nyuma. Naitazama Man City nao watakupa nafasi. Nadhani Liverpool wana nafasi zaidi ya kushinda Ligi ya Mabingwa kuliko Ligi Kuu England," **Nguli wa zamani wa Arsenal, Paul Merson akitoa utabiri wake.**



"Ni mchezaji wa daraja la juu - mchezaji rahisi zaidi kumfundisha kwa sababu mambo yote anayofanya ni ya kawaida kwake. Hakuna haja ya kumfundisha sana. Bila shaka anahitaji kufanyia kazi jambo moja au mawili tunayofanya kwa kujilinda, lakini ana akili sana katika soka, ana roho nzuri na anataka kupigana kwa bidii kwa ajili ya timu," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp akimzungumzia nyota wa kikosi hicho, Luis Diaz baada ya kuonyesha kiwango bora dhidi ya West Ham Jumamosi.**



# PENALTI ZINAVYOGEUKA SOMO GUMU SIMBA



KAGERE

**Na Adam Fungamwango**

UNAWEZA kusema kuwa somo la upigaji wa penalti kwa wachezaji wa timu ya Simba bado ni gumu, kwa sababu licha ya makocha Pablo Franco na msaidizi wake, Selemani Matola mara kwa mara kudai wanalifanyia kazi, lakini hali bado iko pale pale.

**Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ilikosa penalti nyingine, ikiwa ni mlolongo wa penalti nyingi inazokosa msimu huu kuliko kupata.**

Alikuwa ni Meddie Kagere aliyeikosesha Simba kuweza kufunga bao la nne kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Biashara United, akipiga kizembe na kudakwa na kipa James Ssetuba, mechi ikaisha kwa ushindi wa mabao 3-0.

Ilikuwa ni penalti ya sita msimu huu kwa Simba kukosa kati ya 10 kwenye mashindano yote ambayo imebahatika kuzipata.

Lakini inakuwa ni penalti ya tano kwa Simba kukosa kwenye mechi za Ligi Kuu kati ya saba ambazo imezipata.

Simba imefanikiwa kufunga penalti zake nne, mbili kwenye Ligi Kuu, moja Ligi ya Mabingwa Afrika na moja kwenye mechi ya Kombe la Mapinduzi.

Rally Bwallya alifunga bao pekee kwenye mechi ya Ligi Kuu kati ya Simba dhidi ya Polisi Tanzania, Oktoba 27, mwaka jana, mechi ikiisha kwa bao 1-0, na Kagere ambaye alikosa Ijumaa iliyopita, akifunga tuta kwenye mechi ya Ligi Kuu, Februari 3, mwaka huu dhidi ya Prisons na kuwa bao pekee Simba ikishinda, mechi zote zikichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kagere, alifunga penalti Januari 13 kwenye fainali za Kombe la Mapinduzi dhidi ya Azam na bao hilo pekee liliipa ubingwa Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Na Shomari Kapombe alifunga penalti kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas, Februari 13, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ikishinda mabao 3-1.

Zifuatazo sasa ni penalti ambazo wachezaji wa Simba wameshindwa kuziweka nyavuni msimu huu...

**#1. BOCCO (SIMBA VS BIASHARA UNITED)**

Nahodha wa Simba John Bocco ndiye aliyeanza kuitia 'gundu' timu yake, baada ya kukosa mkwaju wa penalti kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu dhidi ya Biashara United, iliyochezwa Septemba 28, mwaka jana kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Ilikuwa ni kwenye dakika ya tano ya nyongeza, wakati kiungo Pape Sakho alipoangushwa eneo la hatari. Bocco ambaye alikuwa anaaminika kuwa ndiye mpigaji bora zaidi kwenye kikosi hicho alipiga juu kidogo kulia kwa kipa James Ssetuba, ambaye aliruka huko huko na kuupangua. Ikawa ni alama ya hatari kwa wachezaji wa timu hiyo msimu huu. Mechi iliisha suluhu.

**#2. NYONI (SIMBA VS RUVU SHOOTING)**

Ilikuwa ni Novemba 19, mwaka jana, Uwanja wa CCM Kirumba, Simba ikishinda ambao 3-1, lakini ikawa siku ambayo ilikosa penalti ya pili, iliyopigwa na mchezaji mwingine wa timu hiyo ambaye naye anaaminika kuwa ni mpigaji mzuri wa matuta, Erasto Nyoni.

Denis Kibu aliangushwa ndani ya eneo la hatari dakika ya 70, Nyoni akaenda kupiga kushoto kwa kipa Mohamed Makaka, akaifuata na kupangua.

**#3. BWALYA (SIMBA VS AZAM)**

Alikuwa ni Sakho tena, aliyeangushwa ndani ya eneo la hatari kwenye mechi iliyochezwa mwaka mpya, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kati ya Simba dhidi ya Azam FC.

Ni mechi ambayo Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-1. Kabla mabao hayajapatikana, tuta lilipatikana dakika ya 13. Bwalya kwa sababu alikuwa ndiye mchezaji pekee aliyefunga kwenye mechi dhidi ya Polisi Tanzania, akaachiwa jukumu hilo. Kwa mshangao wa wengi, alipiga penalti dhaifu, upande wa kushoto mwa kipa Ahmed Aal Salula, akaudaka, ukamponyoka, kwa sababu haukuwa na nguvu, akaudaka tena.

**#4. MORRISON (SIMBA VS RED ARROWS)**

Bernard Morrison, aliingia kwenye kitabu cha wachezaji wa Simba waliokosa penalti msimu huu. Na yeye ndiye anayeweka rekodi ya kukosa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Ilikuwa ni Novemba 28, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, iliyoisha kwa Simba kushinda mabao 3-0. Hassan Dilunga alichezewa vibaya kwenye eneo la hatari na mwamuzi akaamuru tuta dakika ya 29.

Morrison hakupiga kwa ufundi wowote, tena akimwonyesha kipa Charles Kalumba kuwa atapiga wapi, na kweli akapangua.

**#5. MUGALU (SIMBA VS MBEYA CITY)**

Nadhani hii ndiyo penalti iliyowauma zaidi wanachama na mashabiki wa Simba kuliko zote. Kwa sababu ukiangalia penalti zote ambazo ilikosa, haikupoteza mechi zaidi ya hii.

Ilikuwa ni Januari 27, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Mbeya City.

Beki Juma Shemvuni aliunawa mpira golini na mwamuzi akaamuru mkwaju wa penalti. Ilikuwa ni fursa ya Simba kusawazisha bao. Chriss Mugalu alikwenda kupiga kulia kwa kipa Deogratius Munishi 'Dida'. Ni kweli alipotea na kuruka kushoto, lakini mpira ulikwenda kugonga nguzo ya pembeni na kurejea uwanjani, mechi ikaisha Mbeya City kushinda bao 1-0.

**#6. KAGERE (SIMBA VS BIASHARA UNITED)**

Pamoja na kupata penalti kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Azam na pia kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Prisons, Kagere aliikosesha Simba bao, alipopiga penalti iliyodakwa na kipa Ssetuba, ikiwa ni ya pili kwa timu hiyo kukosa dhidi ya Biashara United msimu huu, huku kipa huyo raia wa Uganda akiokoa zote hizo, pamoja na ile ya Bocco, mwanzoni mwa msimu.

**JE, WAJUA?**



KATIKA jumla ya mechi 700 ambazo Manchester United imeshinda tangu kuanza kucheza Ligi Kuu England hadi sasa, nyota wa zamani wa klabu hiyo, Ryan Giggs ndiye mchezaji pekee aliyehusika katika kushinda mechi nyingi zaidi, akishinda mechi 407 kati ya 632 alizocheza, akifuatiwa na Paul Scholes (aliyeshinda mechi 321).



# TARI yapewa siri ya kuinua kilimo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kufanya kazi kwa ufanisi ili kusaidia Tanzania kufikia malengo yake ya kuinua sekta hiyo kiuchumi.

Mavunde aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea makao makuu ya TARI yaliyoko Makutupora jijini hapo.

Alisema serikali imedhamiria kuimarisha utafiti wa kilimo nchini na kuwajengea uwezo watafiti ili kufanya kazi zao kwa ufanisi.

"Miongoni mwa mambo yaliyofanywa ni kuongeza bajeti katika eneo la utafiti ili kukuza sekta ya kilimo nchini, mimi na Mheshimiwa Waziri wetu Bashe ni waumini wakubwa sana wa sayansi ya kilimo, kilimo ni sayansi, kilimo cha nchi yetu hakiwezi kuendelea pasipo kuwekeza kwenye utafiti na kuwajengea uwezo watafiti wetu," alisema.

Mavunde alisema taasisi hiyo ni moyo wa kilimo nchini, hivyo isipofanya vizuri sekta hiyo haitakua.

"Msipofanya kazi nzuri sekta hii haiwezi kukua, hivyo nchi kushindwa kufikia malengo yake tuliyojiwekea ya kukuza uchumi, kuongeza nafasi za ajira na kupunguza umaskini wa Watanzania," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema kutokana na hali hiyo, serikali iliona umuhimu wa kuimarisha utafiti ili kuzalisha mbegu bora na ugunduzi wa mbegu bora ili kuzalisha kwa tija.

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Dk. Geofrey Mkamilo, aliishukuru serikali kwa kulipa umuhimu eneo la utafiti ambapo mwaka 2020/21 walitengewa Sh. bilioni 7.3 na mwaka 2021/22 imeongezeka na kufikia Sh. bilioni 11.6.

Alisema kwa kipindi hicho TARI imegundua aina tano za mbegu bora za mazao ambapo mbili ni za ngano, moja ya mpunga na mbili za choroko.

# CCM, serikali walivyomlilia Mzee Kova

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Philip Mangula, ameongoza mamia ya wakazi wa Wilaya ya Kondoa kwenye maziko ya aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hiyo, Mohamed Kova, huku akisema chama kimepoteza kiongozi bora.

Akizungumza wakati akitoa salamu za chama juzi, Mangula alisema: "Mungu wa ajabu sana zimepita siku 30 tu tangu nilipokutana na Kova enzi za uhai wake na alinitania kwa sababu nilikuwa mwalimu wake wa Chuo cha Uongozi Kivukoni wakati alipoteuliwa kushika wadhifa wa katibu tarafa."

Aidha, Mangula alisema Kova enzi za uhai wake alikuwa kiongozi na mwanasiasa mkomavu na sasa amemaliza safari yake ya duniani na ameondoka na heshima yake.

Kadhalika, aliwataka wanachama wa wilaya hiyo kuendeleza mema aliyokuwa akifanya wakati wa uhai wake.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akitoa salamu alisema Mzee Kova atakumbukwa kwa mambo mengi hasa katika chama na serikali.

"Kova amelala tunahubiri ujenzi wa misikiti, madarasa na vitu vingi, naomba msiba huu uwe funzo kwetu tuhakikishe tunafanya mambo mazuri ili siku unapokufa unawapunguzi viongozi wa dini kutunga uongo katika mahubiri ya msiba wako," alisema Mtaka.

Mtaka alisema serikali pamoja na chama kimepoteza mtu ambaye matendo yake yataishi milele.

Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Dk. Hamis Mkanachi, alisema msiba huo ni mkubwa na ni pigo kubwa kwa sababu wamepoteza kiongozi mahiri na mzalendo.

Alisema Kova alikuwa kiongozi ambaye alizifanya kazi zake kwa weledi, hivyo maono yake na falsafa zake zitaendelea kuishi milele na wanamwombea kwa mwenyezi Mungu ampumzishe kwa amani.

"Msiba huu ni mkubwa na Kondoa tumepata pigo kwa sababu tumepoteza kiongozi mahiri ambaye aliipenda nchi yake na kufanya kazi kwa uzalendo na tunamwombea kwa mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele amina," alisema.

Mtoto wa marehemu Ibrahim Kova akisoma wasifu wa baba yake, alisema amepita katika ngazi mbalimbali za uongozi na hadi umauti ulipomkuta alikuwa ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kondoa.

"Mzee Kova wakati wa uhai wake amelitumikia Taifa katika nyazifa mbalimbali za uongozi ukiwamo wa CCM na serikali na alikuwa mzalendo, tunamwombea kwa Mungu apumzike kwa amani," alisema.

Akitoa salamu kwa niaba ya familia, mdogo wa marehemu, Suleiman Kova, alisema: "Nashukuru Makamu Mwenyekiti Mzee Mangula kwa kuja kuungana nasi katika kipindi hiki kigumu ...nakumbuka juzi usiku saa nane kaka alinipigia akasema anaumwa sana na kwa hali ilivyo anaona kuwa hatapona, hivyo amepiga kuniaga na kunikabidhi kuilea familia ya Mzee Kova kwa sababu mie ndiye nilikuwa Makamu Mwenyekiti wa familia."



Mkazi wa Kijiji cha Bahi Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Maria Lameck, akichota maji katika kisima cha kienyeji walichokitengeneza wananchi wenyewe kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kamati kuhamasisha upishaji ujenzi soko

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, kuunda kamati itakayo shughulikia mchakato wa kuwahamisha wafanyabiashara wa soko la Sabasaba zaidi ya 7,000 ili kupisha ujenzi wa soko la kisasa.

Mtaka aliyasema hayo katika kikao na wafanyabiashara hao chenye lengo la kujadiliana namna mchakato wa kuhamishwa utakavyofanyika kwa kufuata utaratibu maalumu.

Alisema wafanyabiashara wa soko hilo ambao ni zaidi ya 7,000 wapewe taarifa ya kuhamishwa kabla ya miezi nne ya kupisha ujenzi huo.

"Huu mchakato itaundwa kamati itakayoshirikisha wafanyabiashara hao Jiji na ofisi ya Wilaya lengo likiwa ni kuondoa migongano baina ya wafanyabiashara wa serikali ya mkoa huo," alisema.

Alisema kabla ya mchakato wa kuhamishwa wafanyabiashara hao utafanyika upya usajili na kwamba atakayekutwa kwenye sehemu yake ya biashara ndiye atakayesajiliwa.

"Najua kuna watu hawapendi huu mchakato ni kwa kuwa wanamiliki vibanda vingi ambavyo wamevipangisha na wanapokea kodi," alisema Mtaka.

Alisema kamati hiyo itajadiliana katika vikao vyao vya ndani na kupendekeza sehemu tatu ambazo wafanyabiashara hao wataenda kukaa kwa muda ili kupisha ujenzi wa soko hilo.

Aliongeza kwamba baada ya kupendekeza maaeneo hayo kamati hiyo itarudi kujadiliana na wafanyabiashara hao.

Alisema Jiji la Dodoma linakua kwa kasi kubwa katika maendeleo ili kuendana na kasi hiyo ni vema wafanyabiashara wakafanya biashara zao katika mazingira yenye hadhi ya jiji hilo.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, aliwaomba wafanyabiashara hao kutokuwa wabishi kupisha ujenzi huo muda utakapofika.

Alieleza kuwa kila mfanyabiashara atapata nafasi, kizimba cha kufanyia biashara kwa muda na baada ya ujenzi wa soko hilo la Sabasaba kukamilika kila mtu atarudi katika nafasi yake.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wenzake, mfanyabishara, Stephane Massawe, alisema wao hawajagoma kuondoa lakini wanaomba taarifa kuwa ni lini wanaondoka katika soko hilo kupisha ujenzi huo.





## Fedha zatengwa kukamilisha madarasa, vyoo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHILINGI milioni 100 zimetengwa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa ajili kukamilisha ujenzi wa madarasa matatu na matundu ya vyoo 24 katika Shule ya Sekondari ya Iganjo.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Triphonia Kisiga, alisema ujenzi huo utakamilika ndani ya siku 28 ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Mbunge wa Jimbo la Mbeya, Dk. Tulia Ackson ambaye alifika katika shule hiyo na kueleza kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wa shule hiyo.

Dk. Tulia alieleza kuchukizwa na kitendo cha ujenzi wa shule hiyo kusuasua na kuitupia lawama Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Nilitembelea shule hii mwaka jana na kuwaomba ujenzi ukamilike kwa wakati, lakini cha kushangaza hadi sasa ujenzi bado haujakamilika nawaagiza ujenzi wa majengo haya kukamilika haraka maana haiwezekani tuombe fedha na tupatiwe, lakini tusikwamishwe na watu wazembe alisema Dk. Tulia.

Baada ya kauli hiyo Kisiga alimwomba radhi Dk. Tulia na kumwahidi kuwa ujenzi huo utakamilika Aprili mosi huku kukiwa na samani katika vyumba vya madarasa na kufafanua kuwa ujenzi wa madarasa hayo utagharimu Sh. milioni 60 na matundu 24 ya vyoo Sh. milioni 40.

# Watoto kupewa chanjo kuwakinga polio

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imepanga kuanza kutoa chanjo ya ugonjwa wa polio kwa watoto wenye umri wa kuanzia miaka sifuri hadi 15 kuwakinga na ugonjwa huo.

Mratibu wa chanjo mkoani hapa, Danford Barnabas, alisema utoaji chanjo utaanza Machi 21 na wahudumu wa afya watapita nyumba kwa nyumba kwa utekelezaji.

Alisema wamefikia uamuzi huo ikiwa ni jitihada za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa polio ambao tayari umeripotiwa katika nchi jirani ya Malawi.

"Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa maeneo yanayopakana na nchi jirani ya Malawi kwa upande wa Tanzania, tayari mtu mmoja amesharipotiwa kuwa na ugonjwa huo katika nchi hiyo, ikumbukwe kuwa ugonjwa huo ni hatari hauna tiba hivyo ni lazima tukachukua tahadhari za mapema ili kukabiliana na ugonjwa huo moja ya jitihada na kuwachanja watoto wetu ili wasipate madhara," alisema Barnabas.

Alisema licha ya kuandaa utaribu wa kuwafikia watoto wote mkoani Mbeya kupata chanjo, aliitahadharisha jamii yeyote atakayeona dalili za kupooza katika moja ya sehemu ya viungo vyake afike katika kituo cha afya kwa uchunguzi zaidi.

Aliwakumbusha wananchi kuzingatia usafi ikiwa ni pamoja na kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni na usafi wa vyakula kwa kuwa ugonjwa huo unaambukiza kwa njia ya chakula.

Alisema hadi sasa zaidi ya sampuli 20 zilipimwa katika maabara kubaini vimelea vya ugonjwa huo na wote waliopimwa hawakukutwa na ugonjwa huo.

Alisema Mkoa wa Mbeya wataendelea kutoa elimu kwa wananchi namna ya kukabiliana na ugonjwa huo hususani kuhimiza usafi wa mazingira na chakula ili ugonjwa huo usiripotiwe nchini.

"Kwa zaidi ya miaka 15 nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki hazijaripotiwa ugonjwa huo, lakini kipindi hiki tumeona wenzetu wa Malawi, hatuna budi kuchukua hatua za makusudi kwa sababu Tanzania inapakana na nchi hiyo katika mikoa ya Mbeya na Songwe," alisema.

Baadhi ya wanahabari walioshiriki mafunzo ya kuandika habari za chanjo mkoani hapa akiwamo Hobokela Lwinga alisema jamii inapaswa kupewa elimu hiyo haraka ili kuwakinga watoto dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema suala lingine ni wahudumu kwa afya ngazi ya jamii kuhakikisha wanawahamiza kinamama kuwapeleka kwenye vituo vya afya au maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya utoaji wa chanjo kwa kuwa watoto wanaweza kuwa kwenye hatari kubwa ya kupata ugonjwa huo.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, akimkabidhi fedha mmoja wa watu wenye ulemavu ili zikamsaidie kukidhi mahitaji yake, juzi katika kongamano la uwezeshaji kiuchumi wanawake wa Mkoa wa Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mil. 78/- kuwezesha mitaji wanawake wajasiriamali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHILINGI milioni 78, zimetolewa na Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa ajili ya kuwawezesha mitaji wanawake wajasiriamali zaidi ya 600 kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya kupitia Taasisi yake ya Tulia Trust.

Wajasiriamali wanawake wanaofanya biashara zao sokoni kila mmoja alipatiwa mkopo wa Sh. 100,000 ili ukamsaidia kukuza na kuendeleza biashara yake.

Akizungumza na wanawake wa mkoa huo katika siku ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, alisema lengo lake ni kuona wenzake wanajikwamua kiuchumi kupitia shughuli mbalimbali badala ya kubaki nyuma wakilalamika kukwamishwa na mtaji.

Alisema ni mara ya pili sasa anawakusanya wanawake mkoani humo katika viwanja vya Ruanda Nzovwe, kuwapatia mikopo ya kuinua biashara zikiwamo za chakula na bidhaa za majumbani.

"Mimi mbunge wenu ninawapenda sana mara kwa mara nimekuwa nikijitahidi kuwatafutia fedha ili muweze kujikwamua na umaskini kwa sababu sasa hivi wanawake tunaonyesha jitihada kubwa kujipatia maendeleo wengi wenu mmenufaika na mikopo ya vikundi kupitia taasisi yetu ya Tulia Trust, lakini mmoja mmoja amepewa mkopo kwa utaratibu maalum," alisema Dk. Tulia.

Alisema uwezeshaji wanawake kiuchumi mkoani Mbeya ni endelevu na kila mwanamke mjasiriamali atafikiwa na fursa hiyo, muhimu ni kuhakikisha fedha hiyo inatumika kwa lengo lililokusudiwa la kuinua biashara yake.

Vile vile, alisema kwa mwaka jana asilimia 75 pekee ya wanawake waliopatiwa fedha ndiyo waliweza kuinua biashara zao huku asimilia 15 wakishindwa kukuza na kutumia pesa hizo kwa shughuli nyingine, aliwaasa kinamama kujikwamua na umaskini kupitia fursa hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, aliipongeza Taasisi ya Tulia kwa kuandaa utaratibu huo wa kuwaweza kiuchumi wanawake wajasiriamali ambao kutokana na ukata wa fedha walishindwa kuboresha biashara zao.

Alisema baada ya kupatiwa fedha hizo ana imani kubwa kwamba wanawake wa Mkoa wa Mbeya wanakwenda kubadilisha uchumi wa mkoa kwa kuwa watakuwa na mitaji ya kutosha na watalipa ushuru bila tatizo ili kuchangia shughuli za maendeleo.

Alimwahidi Spika, Dk. Tulia kwamba katika kuunga mkono jitahada za kuwawezesha wanawake kiuchumi Wilaya ya Mbeya itaendelea kuwapatia mikopo ya kuwasaidia kuinua na kukuza biashara zao.

Hadi sasa jumla ya wanawake 901 wa Mkoa wa Mbeya kila mmoja amepatiwa Sh. 100,000 kwa ajili ya kukuza biashara yake wanawake 300 mwaka 2021 walipewa fedha na 601 mwaka 2022 walinufaika pia.





Makamu wa Pili wa Rais akizungumza katika uzinduzi wa makala ya hazina ya kutangaza vivutio vya utalii Mkoa wa Kaskazini Unguja iliyofanyika katika hoteli ya Tui Blue Bahari Zanzibar, iliyoko Pwani Mchangani mkoani humo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ma-RC watakiwa ubunifu kutangaza uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wakuu wa mikoa kuwa wabunifu katika kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji na utalii ili nchi ipate mapato.

Hemed aliyasema hayo jana katika hafla ya uzinduzi wa makala ya hazina ya kutangaza vivutio vya utalii Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema Zanzibar inajivunia vivutio vingi vya kitalii ndani ya Mkoa wa Kaskazini ambavyo vinaitangaza nchi kitaifa na kimataifa hatua ambayo inasaidia kuvutia watalii na wawekezaji kuja kwa maslahi ya Taifa.

Hemed alisema kuandaliwa kwa makala hiyo kutasaidia kukuza uchumi wa nchi pamoja na kuvisaidia vizazi vijavyo viweze kufahamu mazingira mazuri yanayoizunguka nchini yao.

Aidha, aliwataka wakuu wa mikoa wengine kuwa wabunifu katika mikoa yao kwa mujibu wa mazingira waliyonayo kwa lengo la kuisaidia serikali katika kukuza uchumi wa nchi hasa eneo la uchumi wa bluu.

Alisema licha ya kutangaza vivutio hivyo, ni vyema kuendeleza mila, silka na tamaduni ili wageni wazidi kuvutiwa na uzuri huo na kufika Zanzibar kwa utalii na uwekezaji.

Pia aliwataka Wazanzibari kuwa mabalozi wa kuitangaza makala hiyo ili iwafikie wengi kujionea vivutio vilivyoko Zanzibar.

Hemed aliupongeza uongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuanzisha makala hiyo ambapo imesaidia kuitangaza Zanzibar.

Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Muhamed Mahmoud, alieleza kuwa mkoa umebarikiwa kuwa na vivutio vingi na miundombinu ya kitalii jambo ambalo limesababisha kuanzisha kwa makala hiyo ili kusaidia kuwafikia wengi ndani na nje ya nchi kuifahamu Zanzibar.

Alisema miongoni mwa mambo yaliyomo katika Mkoa huo ni eneo la sekta ya uchumi wa bluu akitolea mfano utalii, uvuvi, ukulima wa mwani, gesi na mafuta.

Akitoa taarifa ya kitaalamu kuhusu makala na tovuti hiyo Katibu Tawala Mkoa wa Kaskazini Unguja, Makame Machano Haji, alisema kuandaa kwa makala hiyo ni kutekeleza agizo la Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alilolitoa wakati akiwaapisha wakuu wa mikoa ambapo aliwataka kuwa wabunifu katika maeneo yao ya kazi ili kusaidia kukuza uchumi wa nchi.

# SMZ kushirikiana na Shirika la Afrika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto imesema iko tayari kushirikiana na Shirika la Viongozi wa Afrika katika mambo mbalimbali ikiwamo kuimarisha sekta ya afya.

Akizungumza na ujumbe kutoka Shirika hilo ofisini kwake, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema amefurahishwa na ujio wa ujumbe huo na kuahidi kushirikiana nao ili kuhakikisha sekta ya afya inazidi kuimarika nchini.

Alisema ujumbe huo una lengo la kuisaidia sekta hiyo katika mambo mbalimbali ya kiafya ikiwamo kutokomeza kabisa malaria katika jamii."Ingawa malaria yamepungua kwa kiasi kikubwa nchini na kufikia asilimia moja, lakini ipo haja ya kupunguza ugonjwa huo na kuyaondoa kabisa" alisema.

Aidha, alisema shirika hilo lina mpango wa kusaidia na kupambana na magonjwa yasioambukiza kama shinikizo la damu, kisukari, saratani, na mengine mengine.

Mwenyekiti wa Shirika hilo, Joy Phumaphi, alisema lipo tayari kuhamia Zanzibar na kufanyakazi na Wizara ya Afya katika kulinda afya za wananchi wa Zanzibar.

Aliahidi kutoa ushirikiano na Wizara ya Afya ya Zanzibar katika kupunguza vifo kwa wanawake na watoto.

# Othman awakumbusha viongozi majukumu yao

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo, Othman Masoud Othman, amewataka viongozi wa ngazi mbalimbali kujitahidi kusimamia vyema majukumu yao ya kuwatumikia watu.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo jana katika ziara yake ya kichama ya kuyatembelea majimbo ya Kijini na Nungwi mkoa wa Kasikazini Unguja.

Alisema viongozi wote kuanzia wa matawi, majimbo, mikoa hadi Taifa wana wajibu wa mkubwa wa kuhakikisha wanashirikiana vyema na wananchi na kusimamia ipasavyo majukumu yao na huko ndiko kutakakowafanya wananchi na wanachama kujenga imani na viongozi ya kupata matarajio yao ya kuwachagua.

Akizungumzia suala la Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) Zanzibar, Othman alisema chama hicho kimeingia katika serikali hiyo ili kusaidia kujenga na kutengeneza kwa pamoja mfumo bora wa kuendesha nchi.

Alifahamisha kuwa hatua hiyo ni muhimu kwa kuwa itasaidia kutengeneza mazingira sahihi ya ushirikiano wa kuleta mageuzi katika mfumo kuendesha serikali ya Zanzibar, na kwamba chama hicho kimeshawasilisha mapendekezo kadhaa serikani yakishauri kuwapo mabadiliko ya katika maeneo mbalimbali, likiwamo suala utaratibu wa uchaguzi.

Akizungumzia suala la sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti mwaka huu, Othman alisema ni jambo muhimu na kuwataka wananchi wote wasipuuze jambo hilo na kuwa tayari kuhesabiwa muda utakapofika.

Naye Mwenyekiti wa ACT Jimbo la Kijini, Mcha Khamis, aliwataka wanachama wa chama hicho kuendelea kushirikiana kuimarisha chama kwa kuunganisha wanachama wapya kama mwongozo wa chama hicho unavyoelekeza.

Mapema katika ziara hiyo Othman aliweka mawe ya msingi ya matawi mapya matatu ya Jimbo la Kijini pamoja na kuzindua tawi jipya la Mwanahayanza huko Matemwe Kigomani pia alitembelea na kusikiliza wananchi wenye mgogoro wa aridhi kati yao na na muekezaji huko Mbuyu Tende Matemwe na kuahidi kwamba ataliwasilisha kwa Rais jambo hilo ili lipatiwe ufumbuzi.

# Watoto 2 wadaiwa kufa kwa kutumbukia kisimani

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

WATOTO wawili waliotambulika kwa majina ya Samia Hassani na Shafii Ahmadi wa Kijiji cha Mwembetogwa kitongoji cha Kiyanga mkoani Mtwara wamefariki dunia wakidaiwa kutumbukia kisimani wakati wakicheza kando kando ya kisima hicho.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, ACP Nicodemus Katembo, amethibitisha kutokea kwa tujio hilo na kueleza kuwa lilitokea mwishoni mwa wiki katika kitongoji cha Kiyanga, kijiji cha Mwembetogwa mkoani Mtwara.

Kamanda Katembo alisema kabla ya kukutwa na mauti watoto hao waliondoka nyumbani kwao na kwenda kucheza majira ya saa 5 asubuhi na walikuwa wakicheza karibu na kisima hicho.

Alisema wakati wakicheza kando ya kisima ndipo wanadaiwa kutumbukia katika kisima hicho na kupoteza maisha.

Kamanda Katembo alisema ilipofika majira ya mchana wazazi wao walianza kuwatafuta kwa ajili ya kuwapatia chakula ila juhudi za kuwapata ziligonga mwamba.

Alisema kuwa walipoendelea kuwatafuta walifanikiwa kuziona nguo zao zikiwa kando ya kisima hicho, kinachojulikana kwa jina Nembo.

Kamanda Katembo alisema wazazi na walezi wanapaswa kuwa karibu na watoto wao ili kuhakikisha wanawatunza kwa ajili ya usalama wao.



Msomaji maarufu wa Quran duniani kutoka nchini Marekani, Dk. Hassan Saleh, akijiandaa kupanda mche wa mti katika Wilaya ya Kigamboni jijini Dar es Salaam juzi, ikiwa ni jitihada za kuhifadhi mazingira nchini katika kampeni maalum ya Quran na mazingira yenye lengo la kupanda miti 2,000. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Familia yakabidhiwa fedha zinazodaiwa kuombwa na watumishi kituo cha afya

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imekabidhi Sh.150,000 kwa familia ya Jumanne Jackson mkazi wa Ushetu zilizookolewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) zilizoombwa na watumishi wawili wa Kituo cha Afya cha Iboja kwa ajili ya kusafirisha mwili wa marehemu.

Tukio la kutozwa fedha hizo lilitokea mwishoni mwa Desemba, mwaka jana, wakati marehemu, Elizabeth Jackson aliyefika kituoni hapo kujifungua na baadaye alifariki dunia kwa kucheleweshwa kupatiwa matibabu.

Wakati wakijadiliana namna ya kuchukua mwili wa Elizabeth kwa kutumia gari la wagonjwa kumpeleka nyumbani, familia iliombwa Sh.150,000.

Katika fedha hizo inadaiwa mganga mfawidhi wa kituo hicho alichukua Sh. 90,000 na dereva wa gari la wagonjwa Sh.60,000 na walizirejesha baada ya kubanwa na mwijiri wao.

Akikabidhi fedha hizo juzi, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema, vitendo vilivyofanywa na watumishi hao ni kinyume na maadiili ya utumishi wa umma na kwamba watawajibishwa kisheria ili kukomesha vitendo vya namna hiyo katika idara za afya.

Aliwataka watumishi wengine waliohusika katika kuomba rushwa kuwa ni Valency Lazoro mtaalamu wa maabara, Erimikius Leonard, Muuguzi wa Kituo, Ally Joshua Kidelio na Maneno Andrew wote watachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa taratibu za kazi zao.

Alisema, baada ya kufuatilia kwa kina walibaini mgonjwa huyo alipoteza maisha kwa uzembe wa watoa huduma kituoni hapo na gari la wagonjwa lilikuwa zima na lilikuwa na mafuta ya kutosha na iliwezekana kumfikisha katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama kwa matibabu zaidi.

Jumanne Jackson ndugu wa Elizabeth akipokea fedha hizo, alisema, vitendo vya watoa huduma kuwaomba wagonjwa rushwa vimekuwa vikitokea mara kwa mara katika vituo vya afya na zahanati zilizoko pembezoni mwa miji lakini wanakosa namna ya kutoa taarifa.

Alisema, vitendo hivyo vimekuwa vikisababisha wagonjwa maeneo ya vijiji kupoteza maisha kwa kukosa fedha za kuwapatia watoa huduma.

Alisema kwa hali aliyokuwa nayo mgonjwa wao walipaswa kupatiwa huduma kwanza kabla ya kuomba rushwa, hivyo serikali iwachukulie hatua wote waliohusika.

Naye Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema, idara ya afya katika Halmashauri ya Ushetu bado ni tatizo ambalo linahitaji usimamizi wa ili kuondoa shida ambazo zinawakabili wananchi wanaofikia vituo vya afya kupata huduma za kiafya.

Alimtaka Mganga Mkuu wa Halmashauri, Nicodemus Senguo kwa kushirikiana na Mkurugenzi, Linno Mwageni kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wanaobainika kufanya vitendo vya namna hiyo ili kuondoa tatizo la wagonjwa kupoteza maisha kwa kukosa fedha za rushwa.

# DC ampongeza Samia ujenzi kiwanda cha gesi

**Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kujenga kiwanda cha kuzalisha hewa ya oksijeni mkoani Shinyanga.

Ujenzi wa kiwanda hicho kutamaliza tatizo la kwenda jijini Mwanza kujaza hewa hiyo kwenye mitungi kwa ajili ya tiba kwa wananchi.

Alitoa pongeza hizo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kutembelea kiwanda hicho ambacho kimejengwa eneo la Mwawaza katika Manispaa ya Shinyanga na kipo katika hatua ya mwisho ya ukamilishaji ili kianze kazi.

Alisema kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa corona, walikuwa wakipata shida ya kujaza hewa ya oksijeni kwenye mitungi kwa ajili ya kuokoa uhai wa wananchi.

Alisema walikuwa wakijazia gesi jijini Mwanza, lakini sasa hivi tatizo hilo litaisha na wataanza kujaziwa mkoani Shinyanga.

"Tunamshukuru sana Rais Samia kwa kutujengea kiwanda hiki cha kuzalisha hewa ya oksijeni hapa mkoani Shinyanga, ambacho kina uwezo wa kuzalisha mitungi 200 kwa siku moja," alisema Mboneko.

Aidha, alisema kiwanda kama hicho kitajengwa pia katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mitungi 200 kwa siku na hivyo' kuufanya mkoa huo wa Shinyanga kuwa na uwezo wa kujaza mitungi 400 kwa siku.

Katika hatua nyingine Mboneko, alikagua ujenzi wa hospitali ya magonjwa ya mlipuko, pamoja na maendeleo ya ujenzi wa jengo la chumba cha dharura na mahututi katika Hospitali mpya ya Rufani mkoani Shinyanga akiagiza makandarasi waongeze kasi ya ujenzi na kuzingatia ubora.

Kwa upande wake msimamizi wa ujenzi wa miradi katika hospitali hiyo, Fred Mwakyoma kutoka Wizara ya Afya, alisema kiwanda hicho kipo hatua ya ukamilishaji na walishafanya majaribio ya awali ya kujaza hewa ya oksijeni kwenye mitungi.

Akizungumzia ujenzi wa hospitali hiyo, alisema unaendelea vizuri na upo kwenye hatua nzuri.

**Tunamshukuru sana Rais Samia kwa kutujengea kiwanda hiki cha kuzalisha hewa ya oksijeni hapa mkoani Shinyanga, ambacho kina uwezo wa kuzalisha mitungi 200 kwa siku moja.**

HABARI KIMATAIFA

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE

# Russia yatoa saa chache msaada kiutu

**Kyiv,** UKRAINE



Wakazi wa mji wa Irpin nchini Ukraine, wakiondoka nchini humo, baada ya Russia kuendelea na mashambulizi katika miji mikuu, licha ya wito wa kusitisha mashambulizi ili kupisha raia kuondoka. **PICHA: REUTERS**

RUSSIA ilitoa saa chache na kusitisha vita nchini Ukraine, kutoa fursa kwa makundi ya msaada wa kiutu pamoja na raia kuondoka mji wa Mariupol.

Mji huo wenye watu 450,000, ulioko Bahari ya Azov, kungewezesha makutano kati ya vikosi vya Russia vinavyokuja kutoka Crimea iliyounganishwa, ambayo tayari imechukua bandari muhimu za Berdiansk na Kherson, na vikosi vilivyotangaza kujitenga na vikosi vya Urusi katika Jimbo la Donbass.

Makubaliano ya nchi hizo mbili, yalikuja baada ya Russia kuuzingira mji huo wenye bandari pamoja na mji wa Volnovakha, ingawa Ukraine ililaumu Russia kwa kutotekeleza walichokubaliana.

Wizara ya Ulinzi Russia, imesema mashambulizi dhidi ya miji ya Mariupol na Volnonakha nchini Ukraine yaliendelezwa jana baada ya kukamilisha rasmi muda mfupi wa kusitisha mashambulizi kuruhusu uhamishaji wa kibinadamu.

Hata hivyo, Moscow na Kyiv zametupiana lawama juu ya kushindikana kwa mpango wa kusitisha mapigano ambao ungeruhusu raia kuondoka kutoka kwenye miji ya Kusini Mashariki, iliyozingirwa na vikosi ya Mariupol na Volnovakha.

Raia wa Ukraine waliofanikiwa kuondoka wameingia katika nchi jirani za Poland, Romania, Slovakia na maeneo mengine kutafuta hifadhi.

Awamu ya tatu ya mazungumzo kati ya pande mbili hizo yamepangwa kufanyika leo.

Katika hotuba kwenye televisheni mwishoni mwa wiki, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy, ametoa wito kwa watu wake walio kwenye maeneo yanayokaliwa na wanajeshi wa Russia kuendelea kupambana.

Rais huyo amesema ni lazima Waukraine wapambane kuondoa uovu wa adui yake katika miji yao, akitoa ahadi ya kujenga upya taifa lake.

Rais Zelensky amesema jana, amezungumza kwa njia ya simu na Rais wa Marekani, Joe Biden na kujadili juu ya msaada wa fedha pamoja na vikwazo zaidi dhidi ya Russia katika kipindi ambacho taifa lake linakabiliwa na ongezeko la mashambulizi.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu wa Israel, Naftali Bennett, amekutana na Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz, mjini Berlin kwa lengo la kumpa taarifa ya mazungumzo yake na Rais wa Russia, Vladimir Putin.

Msemaji wa Serikali ya Ujerumani, Steffen Hebestreit, amesema Bennett na Scholz wamekubaliana kuwa na mawasiliano ya karibu na kwamba lengo lao kubwa ni kuvimaliza vita vya Ukraine, haraka iwezekanavyo.

> “Nyumba za makazi na barabara zimeharibiwa vibaya kutokana na mashambulio ya angani. Vikosi vya Ukraine pia vipelipua madaraja katika juhudi za kudhibiti wanajeshi wa Russia, ripoti zinasema kutoka mji huo.

Rais Putin ameonya siku ya Jumamosi kwamba nchi yoyote itakayochukua hatua ya kuifunga anga ya Ukraine, itazingatiwa na Moscow kuwa imeingia kwenye mzozo huo.

Mashambulio ya Russia dhidi ya Ukraine yaingia katika siku ya 12, huku idadi ya wakimbizi ikitarajiwa kufikia karibu watu milioni 1.5.

Serikali ya Ukraine imesisitiza kwa nchi za Magharibi kuchukua hatua zaidi ikiwa ni pamoja na kuiongezea Ukraine silaha zaidi na kuiongezea Russia vikwazo.

Rais Putin ameendelea kuwalaumu viongozi wa Ukraine kwa mashambulizi dhidi yake na kuonya kuwa iwapo wataendelea kufanya wanachokifanya, basi wanatilia shaka mustakabali wa serikali ya Ukraine.

Rais Zelensky amehimiza upinzani, akisema raia wa nchi hiyo wanaendelea kudhibiti miji muhimu ya Kati na Kusini Mashariki mwa Ukraine.

Katika hotuba kwa taifa iliyotolewa kwa njia ya video, alitoa wito kwa raia wa nchi hiyo katika miji iliyotekwa na vikosi, kupigana.

Makundi yanayotaka kujitenga yanayoungwa mkono na Russia katika eneo la Donetsk iliyoko miji ya Mariupol na Volnovakha, wameilaumu serikali ya Ukraine kwa mapigano hayo yanayoendelea.

Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, jana, ametoa wito wa kukomeshwa kwa mzozo huo, akitaka njia za kibinadamu zifunguliwe ili kuruhusu raia kukimbia.



Rais wa Russia, Vladimir Putin.

Mji wa Irpin, ulioko kilomita 20, Kaskazini-Magharibi mwa Kyiv, umekabiliwa na vikosi vya Russia na Ukraine katika siku za hivi karibuni.

Mji huo ni muhimu na wa kimkakati ulioko karibu na uwanja wa ndege wa Hostomel, na msafara mkubwa wa magari ya Russia, yamepiga kambi karibu na mji mkuu.

Nyumba za makazi na barabara zimeharibiwa vibaya kutokana na mashambulio ya angani. Vikosi vya Ukraine pia vipelipua madaraja katika juhudi za kudhibiti wanajeshi wa Russia, ripoti zinasema kutoka mji huo.

Maofisa wa Ukraine wanasema Jumamosi kwamba wanajeshi wa Russia, walilipua sehemu ya njia ya reli kwenye njia ya kuwahamisha kutoka Irpin.

Russia imeitishia Ukraine kwamba atainyima hadhi yake kama nchi huru, ikilinganisha vikwazo vya kimataifa vinavyoikumba na tangazo la vita.

### WHO YASHTUMU MASHAMBULIZI VITUO VYA AFYA

Shirika la Afya Duniani (WHO), limesema takriban mashambulizi sita kwenye vituo vya afya yamefanyika tangu kuanza kwa vita nchini Ukraine, na kusababisha vifo vya takriban watu sita. Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Tedros Adhanom Ghebreyesus, anakumbusha kwamba mashambulizi dhidi ya taasisi za afya yanajumuisha ukiukwaji wa sheria za kimataifa za kibinadamu.

Russia, inajiandaa kufanya mashambulizi dhidi ya Odessa, kwa mujibu wa Volodymyr Zelensky.

“Itakuwa uhalifu wa kijeshi. Itakuwa uhalifu wa kihistoria,” Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky amesema kwenye video kama onyo. Kulingana na Rais Zelensky, askari wa Russia wanajiandaa kufanya mashambulizi ya anga katika mji wa Odessa, Bandari Kuu ya Ukraine, iliyoko katika mwambao wa Bahari Nyeusi.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa Mtandao***

# TIMU ZA TAIFA ZA POOLTABLE ZATINGA NUSU FAINALI ZAMBIA

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU za Taifa za mchezo wa Pooltable Wanaume na Wanawake, zimefanikiwa kuingia nusu fainali ya michuano hiyo ya Afrika inayoendelea nchini Zambia baada ya kuvuka hatua ya makundi kwa kishindo juzi.

Timu ya wanaume imetinga nusu fainali kwa kuzifunga timu ya Kenya 13-9, Uganda 13-8 na Zimbabwe 13 -6.

Hadi gazeti hili linakwenda mitamboni jana, hatua ya nusu fainali ilikuwa tayari inaendelea kwa Tanzania kuvaana na Afrika Kusini wakati nusu fainali ya pili ni ilikuwa ni wenyeji Zambia na Uganda.

**Kwa upande wa wanawake, pia Tanzania ilitarajiwa kucheza nusu fainali dhidi ya Afrika Kusini.**

Kocha wa timu ya Taifa ya Pool, Denis Rungu, mwenye uraia wa Zambia, alitatamba kurudi na ushindi wa kishindo Tanzania kutokana na jinsi alivyoviandaa vikosi vyote viwili vya timu ya wanaume na wanawake.

Katika mahindano hayo yanayotarajiwa kumalizika leo nchini Zambia, nchi saba ndizo zilikuwa zikishiriki michuano hiyo ya Pool Afrika ambazo ni Afrika Kusini, Zimbabwe, Kenya, Uganda, Swaziland, Tanzania na wenyeji Zambia huku zote zikiwakilishwa na timu za wanaume na wanawake.

CHAMBUA...



Kiungo wa Simba, Clatous Chama, akipangua safu ya ulinzi ya Biashara United kabla ya kuifungia timu yake bao la tatu wakati ikishinda 3-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Jumamosi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi Tanzania sasa waivutia kasi Simba

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanikiwa kuichapa timu ya Azam FC bao 1-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya NBC uliochezwa jana katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, benchi la ufundi la Klabu ya Polisi Tanzania limewapa mapumziko mafupi wachezaji wake ili kuwaweka sawa kwa mchezo ujao.

Kwa mujibu wa ratiba, Polisi Tanzania ambayo sasa ipo nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 22, itasubiri hadi Machi 27, mwaka huu itakaposhuka tena dimbani, safari hii ikiikaribisha Simba katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Malale Hamsini, alisema amewapumzisha mpaka kesho Jumanne watakaporejea kuanza tena kujifua kwa mchezo ujao.

"Baada ya kupata ushindi hapo jana [juzi], niliwapa mapumziko mafupi wachezaji mpaka Jumanne, na Jumatano tutaanza safari ya kurudi Moshi mkoani Kilimanjaro," alisema Malale.

Kocha huyo alisema baada ya kufika mkoani humo, moja kwa moja wataanza maandalizi ya mchezo dhidi ya Simba, ambao wataivaa ikitoka Ivory Coast kucheza mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas Machi 20, mwaka huu.

"Matokeo tuliyoyapata ni salamu kwa Simba tutakapokutana nao, hatutawaonea huruma kasi itaendelea kuwa pale pale," alisema.

Aidha, alisema atatafuta mechi za kirafiki katika kipindi hiki kabla ya kuivaa Simba, lengo likiwa ni kuwaweka sawa wachezaji wake kuelekea mchezo huo.

# Azam FC yakiri uzembe kipigo

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania, Kocha Msaidizi wa Azam FC, John Yona (pichani), amekiri kuwa wamefungwa kihalali na tatizo kubwa kwao ni kushindwa kuzitumia nafasi nyingi ambazo wamezipata, tofauti na wapinzani wao.



Azam, ikiwa nyumbani juzi usiku, Uwanja wao wa Azam Complex, ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania, ikiwa ni mechi ya tatu ya Ligi Kuu kushindwa kupata ushindi tangu ilipofanya hivyo Februari 4, mwaka huu, dhidi ya Dodoma Jiji FC kwenye uwanja huo.

"Tumepoteza mechi nyumbani, mpira una matokeo matatu, kushinda, kufungwa na kutoa sare, tumeshafungwa hatuwezi kukaa na kufikiria hili, tumefuta sasa tunaangalia mengine na mechi zinazofuata," alisema Yona.

Alisema sababu kubwa ya kupoteza mechi hiyo ni kwamba wachezaji wao walipata nafasi nyingi tena ndani ya eneo la hatari, lakini walishindwa kuzitumia, huku wenzao wakiitumia nafasi walioipata tena wakiwa nje ya boksi.

"Polisi Tanzania wamepata nafasi moja nje ya boksi wamefunga, lakini sisi tumepata nafasi nyingi tumepoteza, tumeingia kwenye eneo lao la hatari mara nyingi sana, kufunga imekuwa shida kwetu," alisema kocha huyo.

Kipigo hicho kinakuwa cha pili kwa Azam tangu ilipoifunga Dodoma Jiji, huku ikiwa ni mechi ya tatu kucheza bila kushinda.

Ilichapwa mabao 2-0 Februari 22, dhidi ya Biashara United kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, ikatoa suluhu dhidi ya Coastal Union Machi Mosi, mwaka huu kabla ya kukutana na kipigo hicho. Ni kipigo cha sita msimu huu, huku ikiwa iko nafasi ya nne kwa pointi 25.

# Ruvu yaitisha Biashara United kutonesha kidonda

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Ruvu Shooting imetamba kuweka chumvi kwenye kidonda cha Biashara United leo, ambacho hakijapona tangu ilipochapwa mabao 3-0 dhidi ya Simba ijumaa iliyopita, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ruvu Shooting inashuka dimbani kujaribu bahati yao leo kwenye uwanja wake wa nyumbani, Mabatini Mlandizi mkoani Pwani itakapocheza dhidi ya Biashara United, ambayo imedai kuwa itatumia staili ile ile ya Simba kuongeza chumvi kwenye kidonda chao.

Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, amesema maandalizi ya mechi hiyo yamekamilika na wanataraji kupata matokeo chanya.

"Tumekuwa kwenye maandalizi makubwa, dhamira yetu ni kupata matokeo chanya, na hii ni kwa sababu hatuko kwenye nafasi nzuri wala mbaya kwenye msimamo wa Ligi Kuu, lakini tunachotaka ni kupanda juu ya msimamo.

"Tangu kulipocheza mechi dhidi ya Dodoma Jiji, tukatoka sare ya bao 1-1, makocha wetu wamekuwa wakirekebisha makosa ya hapa na pale yaliyojitokeza na hatuna wasiwasi sana na Biashara United, si kwa sababu wamefungwa na Simba, lakini tuliwafunga kule kule kwao bao 1-0, sasa ili kuonyesha sisi ni wababe wao, tutahakikisha tunapata matokeo," alisema Masau.

Timu hizo zinafuatana kwenye msimamo wa ligi hiyo, kutokana na Ruvu Shooting kushika nafasi ya 13 ikiwa na pointi 16 na Biashara United iko nafasi ya 14 kwa alama zake 15.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**POGBA KURUDI JUVENTUS**

JUVENTUS wamewasiliana na wakala wa Paul Pogba, 28, Mino Raiola kuhusu uwezekano wa kiungo huyo wa kati wa Manchester United kurejea Turin msimu ujao. ***(Gazzetta dello Sport)***

**ARTETA KUSAJILI NYOTA**

NYOTA wa Real Sociedad raia wa Sweden, Alexander Isak, 22, na mchezaji wa kimataifa wa England na Everton, Dominic Calvert-Lewin (24), wametajwa kuwa walengwa wa Arsenal baada ya kocha Mikel Arteta kusema kuwa hao ndio watakaopewa kipaumbele kipindi cha usajili wa majira ya joto. ***(Sunday Express)***

**ONANA ATAKIWA WEST HAM**

KLABU ya West Ham inapanga kumsajili kiungo wa kati wa Ubelgiji chini ya umri wa miaka 21, Amadou Onana, 20, kutoka Lille, ambayo inataka zaidi ya pauni 20 ili kumwachia kiungo huyo. ***(Sun on Sunday)***

**WIJNALDUM ANUKIA ATLETICO**

KLABU ya Atletico Madrid inatathmini uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa Paris St-Germain, Gini Wijnaldum, 31, ambaye inasemekana hana furaha hapo Paris. ***(Mundo Deportivo)***

**CHRISTENSEN SAFI BARCA**

MLINZI wa Chelsea na Denmark, Andreas Christensen, 25, amekataa kujiunga na klabu yoyote ya Ligi Kuu England na anakaribia kufikia makubaliano ya mkataba na Barcelona, ambayo imetoa ofa nzuri zaidi ya Bayern Munich. ***(Fabrizio Romano)***

**SAKA HAONDOKI ARSENAL**

KIUNGO wa kati wa England, Bukayo Saka, 20, hana mpango wa kuondoka Arsenal, licha ya Liverpool kuonyesha nia ya kutaka kumnunua nyota huyo. ***(Sun on Sunday)***

**XAVI UHAKIKA KWA HAALAND**

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez anaamini klabu hiyo itashinda kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland, 21. ***(Sun no Sunday)***

**KEPA KUMFUATA SARRI**

KOCHA wa Lazio, Maurizio Sarri amepania kuungana tena na kipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga, 27, mjini Rome, ambapo anapanga kumsajili kipindi cha majira ya joto. ***(Corriere dello Sport)***

**GARNER AWANIWA LEEDS**

LEEDS united huenda wakawasilisha dau la kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United, James Garner, 20, msimu wa majira ya joto, huku Southampton pia wakimfuatilia kiungo huyo wa kimataifa wa England ambaye yuko Nottingham Forest kwa mkopo. ***(Sun on Sunday)***

**EN-NESYRI AGOMBEWA**

ARSENAL na Newcastle United zinamtaka mshambuliaji wa Sevilla na Morocco, Youssef En-Nesyri, 24, ambaye alihusishwa na uhamisho wa kwenda Manchester United Januari. ***(Teamtalk)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP: TUMEBAHATISHA KUIFUNGA WEST HAM

**Tulijua kila kitu kuhusu ugumu na utofauti wao, na kipindi cha kwanza tuliweza kukabili hatari...**

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amekubali kwamba Liverpool walikuwa na bahati kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya West Ham United na kuendeleza presha kwa vinara wa Ligi Kuu England, Manchester City.

'Wekundu' hao walipata ushindi huo mwembamba kwenye Uwanja wa Anfield Jumamosi, shukrani kwa bao pekee la Sadio Mane alilofunga dakika ya 27 wakati sasa wakiwa wamepunguza pengo la pointi tatu dhidi ya vinara hao.

Licha ya kucheza bila ya kiungo nyota, Declan Rice na kumpoteza Jarrod Bowen aliyeumia mapema kipindi cha kwanza, West Ham walionyesha kiwango cha kuvutia zaidi.

**Pablo Fornals alifanya kazi ya ziada kuokoa hatari ya Trent Alexander-Arnold, na walipoteza nafasi mbili za maana wakati Manuel Lanzini na Michail Antonio walishindwa kufunga katika dakika 20 za mwisho.**

Akizungumza baada ya mchezo huo, Klopp alikubali kwamba, timu yake ingeweza kupoteza pointi tatu kirahisi.

"Sijui kama tutaukumbuka mchezo huu kama ni mmoja kati ya michezo muhimu sana. Ulikuwa mgumu, lakini tulifanya vizuri katika kipindi cha kwanza," alisema akiiambia Sky Sports. "Tulijua kila kitu kuhusu ugumu na utofauti wa West Ham, na kipindi cha kwanza tuliweza kukabili hatari zao zote.

"Tungeweza kufunga mabao mengi zaidi, tulishindwa na mchezo ulikuwa wa wazi kabisa. Niliwaambia vijana kama hamjajipanga mnatakiwa kucheza kwa morali kubwa, na ndicho kilichofanyika."


SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
SIMBA
VERSUS
DODOMA FC
1 | 1.29
X | 5.00
2 | 11.00

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANCELOTTI ATAKA KAZI KAZI KWA PSG



**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti anahisi Real Madrid watakuwa na nafasi nzuri ya kuifunga Paris Saint-Germain kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kama wataendelea na kiwango walichoonyesha wakati wakiwafumua Real Sociedad.

'Los Blancos' hao walitoka nyuma kuwafurumusha Sociedad walioko nafasi ya sita kwenye msimamo kwa mabao 4-1 pale katika Uwanja wa Santiago Bernabeu Jumamosi na kuongoza msimamo kwa tofauti ya pointi nane dhidi ya Sevilla katika msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Mikel Oyarzabal aliwapa Sociedad bao la kuongoza kwa mkwaju wa penalti baada ya Dani Carvajal kumfanyia madhambi, David Silva, lakini mabao ya Eduardo Camavinga na Luka Modric yakawarudisha Madrid mchezo.

Karim Benzema alifunga bao lake la 20 kwenye LaLiga msimu huu kwa mkwaju wa penalti baada ya kukataliwa bao lingine kwa kuotea na Marco Asensio akafunga la nne dakika 11 baadaye.

Madrid sasa wana kibarua cha kupindua meza ya bao 1-0 wakati wakiwavaa PSG kwenye mchezo wa pili wa hatua ya 16 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

Kikosi hicho cha kocha, Ancelotti kitakuwa na faida ya kucheza mchezo huo nyumbani, huku vinara hao wa Ligue 1 wakitoka kupoteza kwa bao 1-0 kutoka kwa Nice, Jumamosi.



## Pochettino alia na kiwango

**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino amebainisha kwamba, kipigo walichopata Paris Saint-Germain kutoka kwa Nice kilikuja kama kukosa bahati kuliko kitu kingine chochote, baada ya bao la Andy Delort la dakika za mwisho kuwazamisha vinara hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Jumamosi

PSG ikicheza dhidi ya kikosi hicho cha kocha, Christophe Galtier pale kwenye dimba la Allianz Riviera, ilijikuta ikikukubali kipigo cha bao 1-0, shukrani kwa bao pekee la straika huyo wa Algeria.

Huku Kylian Mbappe akikosekana kwenye mchezo huo, PSG sasa wamepoteza mechi mfululizo wakati wakipambana kuelekea kwenye kubeba ubingwa wa kwanza wa Ligi tangu Aprili mwaka 2019.

Pochettino alibainisha kwamba kikosi chake hakikucheza kwa kiwango cha kutosha ili kupata ushindi, lakini akadai kuwa Nice walipata pointi hizo tatu kwa bahati mbaya.

"Tulifikiri kwamba, tutamaliza mchezo huu kwa sare kwa sababu timu zote hazikuonyesha kiwango cha kutosha kushinda," alisema kocha huyo raia wa Argentina akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# MAYANGA AIPIGIA HESABU GEITA GOLD



Na Shufaa Lyimo

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Mtibwa Sugar, Salum Mayanga, amesema anaivutia kasi timu ya Geita Gold watakayokutana nayo kwenye mchezo ujao wa wa Ligi Kuu ya NBC, utakaopigwa Machi 13, mwaka huu, katika Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mayanga alisema wachezaii wake wanaendelea vizuri na ana matarajio ya kufanya vizuri katika mechi hiyo.

"Baada ya kufanya vizuri kwenye michezo ya ugenini, sasa tunajiandaa kukutana na Geita na mwendo wetu ni ule ule," alisema Mayanga.

Mtibwa imetoka kulazimisha sare tasa ugenini dhidi ya Tanzania Prisons kwenye mchezo uliopigwa Jumatano iliyopita katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Kutokana na matokeo hayo, Mayanga alisema wachezaji wake wanajiamini watapata matokeo mazuri kwenye mchezo huo ujao licha ya msimu huu kuwa mgumu.

Kocha huyo alisema amepata faraja baada ya kuona timu yake haijapoteza mchezo wake wa ugenini.

# Ihefu na matarajio kurejea Ligi Kuu

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Timu ya Ihefu FC, Zuberi Katwila (pichani), amesema ana matarajio makubwa na timu yake kuendelea kupata pointi katika michezo yao ya Ligi ya Championship na kufikia malengo yao ya kurejea kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2022/23.

Ihefu FC ambayo kwa sasa ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi 44, juzi wakiwa ugenini katika Dimba la Azam Complex, Chamazi walikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa DTB FC ambao wana alama 49 kileleni mwa kundi lao.

Ligi hiyo ya Championship imegawanywa katika makundi mawili A na B, na timu zitakazoongoza kila kundi zitapanda moja kwa moja daraja, wakati zitakazoshika nafasi ya pili zitacheza mechi za mchujo dhidi timu mbili zitakazoshika nafasi ya 13 na 14 kwenye Ligi Kuu ili kuwania nafasi mbili za kucheza ligi hiyo msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema ligi hiyo imekuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu inatafuta pointi ili kufikia malengo yao ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao kama ilivyo kwao.



"Tumepoteza mechi ya leo (juzi) dhidi ya DTB FC, imetuongezea hasira za kupambana katika kuhakikisha tunaenda kutafuta pointi muhimu za kufikia malengo yetu," alisema Katwila.

Alisema kubwa ambalo anaenda kulifanyia kazi ni umakini na utulivu wa washambuliaji wake kwa sababu walitengeneza nafasi nyingi katika mchezo huo, lakini safu hiyo ikishindwa kuzitendea haki.

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 07/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1708 | Ruvu Shooting vs Biashara United | 2.65 | 2.80 | 3.05 |
| 14:00 | 2927 | Gokulam Kerala FC vs Real Kashmir | 2.08 | 3.28 | 3.18 |
| 14:00 | 4653 | FC Rotor Volgograd vs Tom Tomsk | 1.77 | 3.41 | 4.13 |
| 15:45 | 1076 | Egnatia Rrogozhine vs Teuta Durres | 3.61 | 2.84 | 2.12 |
| 15:50 | 3662 | Alshoulla vs Al Jabalain | 2.80 | 2.90 | 2.80 |
| 16:00 | 3217 | Arda Kurdzhali vs Beroe | 2.61 | 3.00 | 2.61 |
| 16:00 | 4531 | National Bank vs Misr Lel Makasa | 1.66 | 3.60 | 5.13 |
| 16:00 | 5767 | KMC vs Coastal Union | 2.30 | 2.80 | 3.70 |
| 16:30 | 1667 | MC Magra vs CS Constantine | 3.42 | 2.79 | 2.22 |
| 16:30 | 2151 | Bhayangkara Surabaya Utd vs PSS Sleman | 1.36 | 4.25 | 7.72 |
| 16:30 | 4229 | Zenit St Petersburg vs Ufa | 1.13 | 7.44 | 17.61 |
| 16:30 | 5237 | Rostov vs Sochi | 2.99 | 3.18 | 2.32 |
| 16:30 | 5614 | CR Belouizdad vs Paradou AC | 1.74 | 3.32 | 4.43 |
| 17:00 | 4624 | Tiddim Road Athlectic Club vs Neroca FC | 2.39 | 3.22 | 2.70 |
| 17:00 | 5803 | ATK Mohun Bagan vs Jamshedpur | 2.24 | 3.24 | 2.90 |
| 18:20 | 2635 | Al Qadisiyah vs Ohud Medina | 2.17 | 3.15 | 3.60 |
| 18:30 | 2171 | Ismaily SC vs Farco FC | 2.32 | 3.06 | 3.16 |
| 18:30 | 4286 | Botosani vs Argesul Pitesti | 2.37 | 3.04 | 3.04 |
| 18:45 | 4214 | Kukesi vs Vllaznia | 2.45 | 2.84 | 2.94 |
| 19:00 | 4665 | Simba vs Dodoma FC | 1.29 | 5.00 | 11.00 |
| 19:00 | 5714 | Akhmat Grozny vs Rubin Kazan | 1.86 | 3.39 | 4.02 |
| 20:00 | 1250 | Ahi Nazareth vs Bnei Yehuda | 2.30 | 3.12 | 3.17 |
| 20:00 | 2109 | Gaziantep BB vs Hatayspor | 2.32 | 3.34 | 2.90 |
| 20:00 | 2120 | Ironi Hasharon vs Maccabi Bney Reine | 3.32 | 3.17 | 2.20 |
| 20:00 | 4071 | Kayserispor vs Alanyaspor | 2.43 | 3.34 | 2.75 |
| 20:00 | 4242 | Balikesirspor vs Denizlispor | 3.28 | 3.37 | 2.01 |
| 20:00 | 5321 | Besiktas vs Basaksehir | 2.04 | 3.40 | 3.45 |
| 20:10 | 5320 | Austria Lustenau vs Floridsdorfer AC | 1.83 | 3.52 | 3.71 |
| 20:45 | 2621 | Concarneau vs Le Mans | 1.62 | 3.61 | 5.27 |
| 21:00 | 1135 | TSV Havelse vs Viktoria Berlin | 3.10 | 3.34 | 2.18 |
| 21:00 | 1578 | Vilafranquense vs Rio Ave | 3.32 | 3.32 | 2.07 |
| 21:00 | 2311 | AIK Football vs Orebro SK | 1.19 | 5.80 | 11.60 |
| 21:00 | 3148 | Legia Warszawa vs Slask Wroclaw | 1.74 | 3.46 | 4.23 |
| 21:00 | 3578 | Zamalek vs El Gouna | 1.45 | 4.15 | 6.91 |
| 21:00 | 5207 | Aarhus vs Nordsjalland | 1.82 | 3.59 | 4.04 |
| 21:30 | 2409 | Maccabi Tel Aviv vs Beitar Jerusalem | 1.26 | 5.02 | 9.08 |
| 21:30 | 5101 | Universitatea Craiova vs Farul Constanta | 2.07 | 3.23 | 3.48 |
| 22:00 | 4271 | Jong Utrecht vs Almere City | 2.89 | 3.52 | 2.20 |
| 22:00 | 5003 | Jong PSV vs Emmen | 3.08 | 3.38 | 2.15 |
| 22:00 | 5204 | Jong Ajax vs ADO Den Haag | 2.17 | 3.61 | 2.88 |
| 22:00 | 5567 | Jong AZ Alkmaar vs Telstar | 2.38 | 3.42 | 2.68 |
| 22:30 | 3061 | Nottingham vs Huddersfield | 2.05 | 3.36 | 3.46 |
| 22:45 | 5611 | Toulouse vs Dunkerque | 1.31 | 4.91 | 9.03 |
| 23:00 | 1093 | Athletic Bilbao vs Levante | 1.57 | 4.10 | 5.60 |
| 23:00 | 2804 | Real Sociedad B vs Sporting Gijon | 2.61 | 3.00 | 2.75 |
| 23:00 | 3069 | Virtus Entella vs Carrarese | 1.88 | 3.22 | 4.36 |
| 23:00 | 5048 | Tottenham vs Everton | 1.55 | 4.21 | 5.61 |
| 23:00 | 5993 | Univ San Martin vs Atletico Grau | 2.41 | 3.13 | 2.74 |
| 23:15 | 2217 | Tondela vs Belenenses | 1.96 | 3.40 | 3.69 |
| 23:30 | 2391 | Atletico Huila vs Leones FC | 2.09 | 3.13 | 3.32 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Machi 7, 2022
Nipashe



Klopp: Tumebahatisha kuifunga West Ham

UKURASA 21

HUPITI...



Winga wa Yanga, Denis Nkane, akijaribu kuipenya ngome ya Geita Gold FC wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba hesabu kwa Berkane, Dom Jiji leo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ikishuka Uwanja wa Benjamin Mkapa leo majira ya saa 10:00 alasiri kuivaa Dodoma Jiji FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara ikiwa ni siku sita kabla ya kuikaribisha RS Berkane ya Morocco uwanjani hapo katika mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa miamba hiyo ya soka nchini, Pablo Franco, ametaka kila nafasi bao.

Awali, mchezo huo dhidi ya Dodoma Jiji ulikuwa upigwa saa 1:00 usiku leo, lakini sasa utapigwa saa 10:00 alasiri, hatua ambayo pengine ni hesabu na mkakati wa Simba kuivutia pumzi RS Berkane ambayo wataikaribisha Jumapili ijayo muda huo wa saa kumi.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Pablo alisema kila nafasi watakayoitengeneza hawana budi kuitendea haki kwa kuzamisha mpira kimyani ili kujipunguzia presha na kuweza kucheza mchezo wao waliouzoea wa soka la kurudisha.

Pablo alisema wamekuwa wakifanyia mazoezi ya kutumia vema nafasi wanazotengeneza jambo ambalo anaamini endapo wataweza kuhamisha kile walichokifanyia mazoezi watapata ushindi mkubwa.

"Tumekuwa tukiwasisitiza wachezaji kuhakikisha wanatumia kila nafasi tutakayoipata kwani tunahitaji kufanya hivyo ili kujipunguzia presha na kumudu kucheza mpira wetu tuliozoea.

"Tunatambua mchezo utakuwa mgumu, lakini tumejipanga kucheza vizuri na kushinda, pia tutawatumia wachezaji ambao watakuwa tayari kimwili na kiakili kwa mchezo huo," alisema kocha huyo raia wa Hispania ambaye mchezo uliopita uwanjani hapo alikiongoza kikosi chake kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Biashara United.

# Mayele, Yanga watanua kileleni

### ●●● Afikia mabao ya Lusajo mbio za Kiatu, lakini azua hofu baada ya kuumia, hivyo...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la sekunde ya 40 lililofungwa na straika hatari Fiston Mayele, limewafanya vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga kuzidi kuiweka kwenye nafasi nzuri ya mbio za kuutwaa ubingwa msimu huu, baada ya kuukosa kwa msimu nne.

**Ni bao ambalo limemfanya straika huyo wa Kikongomani kufikisha idadi ya mabao 10, akimfikia straika Mtanzania wa Namungo, Relliants Lusajo, sasa wakiwa wote kileleni kwenye orodha ya wafungaji mabao kwenye Ligi Kuu.**

Hata hivyo, katika mechi hiyo ya raundi ya 17 ya Ligi Kuu, ilichezwa jana jioni kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, Mayele alizua hofu kwa mashabiki wa Yanga baada ya kuumia na kushindwa kumaliza mchezo huo.

Ulikuwa mpira mrefu uliopigwa kutoka nyuma, ukadunda na kuonekana kuwapoteza maboya mabeki watatu wa Geita Gold wakiongozwa na Kelvin Yondani, mpira ukamfikia Mayele ambaye aliwafungasha tena mabeki hao, akaingia kwenye eneo la hatari na kuukwamisha mpira wavuni.

Kama timu zote mbili zingekuwa makini, basi mpaka dakika ya sita mabao yangeweza kuwa 2-2, kwani zote zilianza mpira kwa kasi na kushambulia kwa zamu huku zikipoteza nafasi kadhaa za kufunga.

Dakika ya nne, George Mpole, straika mwenye mabao manane kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu, alikosa bao la wazi akiwa amemlamba chenga kipa Djigui Diarra, lakini akiwa pembeni kidogo, alitaka kufunga mwenyewe na mpira huo ukagusa nyavu za nje.

Dakika moja baadaye Eric Yema, angeweza kuisawazishia Geita Gold, baada ya kuruka kichwa mpira wa krosi akiwa hajakabwa vema na mabeki wa Yanga, lakini kwa mastaajabu akauparaza badala ya kuupiga kichwa ili afunge.

Baada ya Geita Gold kukosa, dakika nyingine moja baadaye, ikiwa ni dakika ya sita, Mayele naye alimlamba chenga kila Aron Kalambo, akiwa pembeni kidogo mwa goli, lakini naye alikuwa mchoyo, kwani badala ya kumpa Feisal Salum aliyekuwa analitazama goli likiwa tupu, akageuka kutaka kupiga mwenyewe na muda huo huo, mabeki wa timu pinzani walimuwahi na kuutoa kona.

Baada ya hapo kasi ilianza kupungua taratibu, lakini Geita Gold wakionekana kutulia na kuwabana Yanga.

Dickson Job angeweza kuandika bao la pili dakika ya 21, aliporuka juu na kuunganisha mpira wa kona iliyopigwa na Deus Kaseke, huku mabeki wa Geita Gold wakishindwa kuruka, lakini haukulenga lango, huku dakika ya 37, Mpole kwa mara nyingine tena, akiikosesha Geita bao, alipoufuma mpira uliokuwa unazagaa langoni mwa Yanga, lakini shuti lake lilimbabatiza kipa Diarra na kurejea uwanjani.

Kipindi cha pili hakikuwa na kashikashi kama cha kwanza, Yanga ikiwatoa Mayele aliyeumia, nafasi yake kuchukuliwa Heritier Makambo, Denis Nkane na Paul Geofrey walitoka, nafasi zao zikachukuliwa na Zawadi Mauya na Dickson Ambundo, huku Geita Gold wakiwaingiza Offen Chikola, Juma Mahadhi na Raymond Mwasota, badala ya Juma Abdallah, Danny Lyanga na Yema, lakini hakukuwa na cha ziada zaidi ya kosakosa.

Geita Gold itabidi ijilaumu yenyewe kwa kushindwa kupata angalau sare kwenye mechi hiyo, kwani ilipata nafasi nyingi zaidi, pamoja na faulo nyingi langoni mwa Yanga, lakini zote zilipotezwa kirahisi na Mpole aliyeongoza kuikosesha timu yake bao, huku lingine likiwa kwenye dakika ya 55, alipopiga kichwa fyongo, baada ya krosi maridadi kutoka kwa David Kameta 'Duchu'.

Yanga sasa imefikisha pointi 45, ikiizidi Simba kwa pointi 11 zaidi, huku Geita Gold ikiwa kwenye nafasi ya nane kwa pointi 21.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >